# Nipashe

Jumatatu Oktoba 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581087

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ

MWANGA WA JAMII

0745 700710

LIKE & FOLLOW US



UNGANA NA BABA LEVO KUPITIA

"kamatacrypto.com"

UPATE BITCOIN AFRICA YA BURE!

wekeza kuanzia $25!



kamatacrypto



JACKPOT BABA LAO!

TZS. 360,499,520

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Majaliwa ataka mkakati wa NMB uwe endelevu

UKURASA 4



# Kibano vigogo wasukaji kesi

• **Serikali** yaandaa orodha ya taasisi, watendaji wanaoitia hasara ya mamilioni... *Endelea Uk. 22*



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa CCM Wilaya ya Amani, Unguja jana. **PICHA: IKULU**

## Mwinyi atangaza mageuzi CCM

UKURASA 2



## Wachumi waona jambo ufadhili wa Samia vyuoni

UKURASA 2


**MICHEZO** **SHAKIRA MAHAKAMANI HISPANIA** UK.27 **KABWELA** UK.7



Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati), akitembelea eneo la mtambo wa kuchakata gesi asilia la Equinor, Norway. Wengine ni Balozi wa Tanzania nchini Nordic, Grace Olotu, Balozi wa Norway nchini Tanzania, Elisabeth Jacobsen na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi aahidi kufanya mageuzi makubwa CCM

**Na Waandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema anatarajia kufanya mageuzi makubwa ndani ya chama atakaposhika nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar mwishoni mwa mwaka huu.

Rais Dk. Mwinyi aliahidi hayo jana baada ya kushiriki uchaguzi wa nafasi mbalimbali za uongozi wa chama ngazi ya Wilaya ya Amani uliofanyika kwenye Ukumbi wa Amani, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Dk. Mwinyi alisema zimebaki hatua mbili za uchaguzi ndani ya chama ambazo ni ngazi ya mkoa na taifa ili kufanya mabadiliko ya uongozi na baada ya kukamilika hatua hizo, atakuwa Makamu Mwenyekiti, akipanga kufanya mageuzi.

Aliwataka wana CCM kuchagua viongozi wenye uwezo na kuacha tabia ya kuchagua kwa kuangalia sura na urafiki, jambo ambalo halitawezesha chama hicho kupata viongozi makini na sahihi.

"Kabla ya mwisho wa mwezi huu (Oktoba) tutakamilisha ngazi ya mkoa na baadaye tutaenda kwenye taifa na tukimaliza taifa maana yake safu imeshapangika timu madhubuti ya kuchukua ushindi 2025, tusifanye makosa, tuendelee kuchagua watu kwa uwezo wao na siyo vinginevyo," alisema na kuongeza:

"Unaweza ukawa na rafiki yako, shoga yako unaweza kuwa na mpenzi wako lakini urafiki tuweke mbali, kwenye chama tunataka watu wenye uwezo... kwa hatua tatu zilizobaki tuhakikishe tunachagua watu wa kutuvusha kwenye uchaguzi ujao ili tuendelee kushika dola."

**UCHAGUZI WILAYANI**

Wakati Dk. Mwinyi akiahidi hayo, Thomas Muyonga ameshinda nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama mkoani Shonyanga kwa kupata kura 1,722, akiwabwaga Costantine Makoye (kura 179) na Michael Kurwa (127).

Msimamizi wa uchaguzi huo, James Kusekwa alitangaza matokea na majina ya waliojitokeza kugombea nafasi mbalimbali ambapo alimtangaza Mwenyekiti Thomas Muyonga kutetea nafasi hiyo, akichaguliwa kuongoza kwa awamu ya pili.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Msanii Richard alimtangaza Magile Makombe kuwa Mwenyekiti wa Wilaya ya Shinyanga Mjini.

Mshindi huyo alipata kura 296 kati ya kura 515 zilizopigwa huku kura moja ikiharibika na kubaki halali 514. Wagombea wengine katika uchaguzi huo na idadi ya kura walizopata kwenye mabano ni Mokhe Warioba (144) na Pendo Sawa (74).

Kwa CCM Wilaya ya Shinyanga Vijijini aliyeshinda nafasi ya Uenyekiti ni Edward Ngelela ambaye alikuwa akitetea nafasi hiyo huku wilayani Kishapu, Shija Ntelezu naye akitetea nafasi hiyo kwa kuibuka mshindi.

Justine Nusurupila alishinda nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Njombe, kwa kura 739, huku Mwenyekiti wa zamani, Edward Mgaya akishindwa kutetea nafasi yake kwa kupata kura 599 na Joyce Gakye kura 22.

Akitangaza matokeo hayo msimamizi wa uchaguzi huo na Mjumbe wa NEC Taifa Mkoa wa Njombe, Fidelis Lumato alisema jumla ya wajumbe ni 1,482 na waliopiga kura ni 1,364 na kura halali ni 1,360.

Katika wilaya za Iramba na Manyoni waliokuwa wenyeviti wametetea nafasi zao katika uchaguzi uliofanyika jana.

Msimamizi wa uchaguzi katika Wilaya ya Manyoji, Mbunge wa Jimbo la Ikungi Mashariki, Miraji Mtaturu, alimtangaza Jumanne Makhanda kuwa mshindi kwa kupata jumla ya kura 1,087.

Makhanda alitetea nafasi yake baada ya kuwashinda wagombea wenzake wawili na kura walizopata kwenye mabano, Grace Mlule (57) na Elia Nollo (27).

Katika Wilaya ya Iramba, Samweli Joel alifanikiwa kutetea nafasi yake kwa kuwashinda Daniel Sima na Elias Mkoma.

Wilayani Siha wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM walimchagua Willfred Mossi kuwa mwenyekiti wa chama hicho kwa awamu ya pili mfululizo.

Mossi alitetea nafasi yake baada ya kupata kura 429 dhidi ya mshindani wake wa karibu Luka Laizer aliyepata kura 15 na mwanamke pekee, Edina Lukumay kuambulia kura 10.

Katika Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba ametetea kiti cha uenyekiti wa CCM wilayani humo akipata kura 871 dhidi ya Moses Mwidete (186) na Tumpale Laizer (5).

Majaliwa Mlawizi ameshinda kwa kupata kura 592 wilayani Mbozi akimwangusha Saimon Mboya aliyekuwa anatetea kiti (383) na Wilison Simbeye (47).

Wilayani Momba, Silvester Lwila ameshinda baada ya kupigiwa kura 580 dhidi ya Simwelu Weston (456), Frank Mbembela (27) na Sophia Mwaijaja (21). Aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM wilayani humo Twaha Maulid, maarufu Twist, hakuchukua fomu ya kuwania uongozi.

Albert Mabrouk ameshinda kuwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Songwe baada ya kupata kura 547 dhidi ya Hamad Juma aliyekuwa anatetea kiti hicho (341) na Fatuma Nkelanza (32).

Wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro, aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Moshi Mjini, Alhaj Omar Shamba, ameshindwa kutetea nafasi yake baada ya kuangushwa na mpinzani wake wa muda mrefu, Faraj Swai.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Msimamizi wa Uchaguzi, Mary Sulle, alisema Swai alichaguliwa kuwa mwenyekiti mpya baada ya kupata kura 308 huku mwenyekiti aliyemaliza muda wake akipata kura 216.

***Imeandikwa na Marco Maduhu (SHINYANGA), Neema Sawaka (KAHAMA), Elizabeth John (NJOMBE), Thobias Mwanakatwe (SINGIDA), Godfrey Mushi (MOSHI) na Nebart Msokwa (MBEYA)**

# Wachumi waona jambo katika ufadhili wa Samia

**Na Romana Mallya**

WATAALAMU wa uchumi na wadau wa maendeleo wamesema ufadhili wa masomo unaotolewa na serikali kwa wanafunzi waliofaulu vizuri masomo ya sayansi kidato cha sita, uliopewa jina la Samia Scholarship, utachangia kupata watu wenye ujuzi na uwezo mkubwa kazini.

Jumanne iliyopita, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitangaza kufunguliwa rasmi tangazo la ufadhili huo huku matokeo ya kidato cha sita mwaka huu yakionyesha wanafunzi 640 ndiyo waliofaulu kwa kiwango cha juu katika masomo ya sayansi.

Alisema endapo watadahiliwa katika masomo ya sayansi, watakuwa wanufaika wa ufadhili huo.

Mchambuzi wa Masuala ya Uchumi, Prof. Haji Semboja, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, alisema ufadhili huo una maana kubwa kwa taifa kwa kuwa utachangia kila wakati kupata watu wenye ujuzi na uwezo mkubwa kazini.

Prof. Semboja alisema ufadhili wa masomo, hasa kwa vijana wa kike, unatoa fursa kwa kundi hilo kujiendeleza zaidi.

"Hii ni jitihada nzuri kwa serikali, mfumo wa maisha wa dunia umebadilika ambapo sera, sheria na taratibu zile za kiubaguzi zimepitwa na wakati au hazipo tena. Watu wasiendelee kufikiria kwamba ipo mifumo kandamizi," alisema.

Alisisitiza jamii imekuwa ikimwangalia mtoto wa kike kwa jinsia yake, lakini kwa wale ambao wametoka nje ya mtandao huo na kuamua kujiendeleza, kwa sasa ndiyo wahandisi na wameshika nafasi mbalimbali kwenye kampuni.

Mchambuzi huyo alitoa wito kwa watoto wa kike kutumia uwezo wao vizuri kupitia fursa wanazopewa na wasilikatishe tamaa taifa, bali wajitahidi kwenye masomo hayo ya sayansi kwa sababu uwezo wao ni sawa na watoto wa kiume.

Katibu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake Hospitali ya Taifa Muhimbili (MHN), Lilian Mnabwiru, alisema zamani iliaminishwa masomo ya sayansi ni magumu na wanayoyaweza ni wanaume, hivyo kuwafanya watoto wa kike kuingiwa na woga wa kuyachukia.

"Juhudi za Mheshimiwa Rais Samia zinaonyesha inawezekana kuwafanya watoto wa kike wasiyaogope masomo kwa sababu wengi wana uwezo.

"Ukiangalia kwa mwaka huu katika matokeo ya kidato cha sita, walioongoza kwenye masomo ya sayansi ni wasichana, tena kwa viwango vya juu, zile nafasi 10 za juu karibu wanafunzi wanane ni wanawake. Mheshimiwa Rais alivyotoa hizo fursa inazidi kuwafanya wahamasike zaidi kuwa inawezekana," alisema.

Dk. Mnabwiru alisema kwa sasa wanawake wanaosomea udaktari na madaktari bingwa mbobevu ni wengi kulinganishwa na miaka 10 iliyopita.

"Tunatoa wito kwa watoto wa kike watumie vizuri fursa hii ya ufadhili wa masomo ya sayansi ili kuhamasisha wengi kupata hizi nafasi, ukipata nafasi na ukafanya vibaya, unafanya aliyeitoa avunjike moyo, wafanye vizuri na kuonyesha ufadhili huo haujatolewa kama hisani kwao, bali ni kwa lengo la kuwainua wao na wengine," alihimiza.

Wakati wa Bunge la Bajeti Mei mwaka huu, Waziri Mkenda, alibainisha kuwa kuanzia mwaka huu, katika kutekeleza juhudi za kukuza sayansi nchini, serikali itatoa ufadhili wa asilimia 100 kugharamia masomo ya chuo kikuu kwa wanafunzi watakaofanya vizuri kwenye masomo hayo katika mitihani ya kidato cha sita.

# Majaliwa ataka mkakati wa NMB uwe endelevu

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameitaka Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya NMB chini ya Mwenyekiti wake, Dk. Edwin Mhede na Menejimenti ya benki hiyo chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna kuendeleza Mbio za Hisani za NMB Marathon licha ya kuvuka lengo la kukusanya Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka miwili.

Mbio za NMB Marathon zilianzishwa mwaka jana kwa lengo la kukusanya Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne (sawa na Sh. mil. 250 kila mwaka) lakini mwitikio chanya ukawezesha kukusanya Sh. milioni 400 mwaka jana na Sh. milioni 600 mwaka huu, hivyo kufikia lengo ndani ya miaka miwili.

Akizungumza wakati wa kutoa shukrani kwa waandaaji, wadhamini na washiriki mwishoni mwa mbio hizo katika Viwanja vya Leaders Club, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Waziri Mkuu Majaliwa alisema baada ya kuvuka lengo hilo, ni wakati sahihi sasa makusanyo yatokanayo na mbio yakaelekezwa kwingine.

"Niipongeze Bodi ya Wakurugenzi NMB chini ya Mwenyekiti, Dk. Edwin Mhede na Menejimenti ya benki hii chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna kwa uratibu wa jambo hili zuri.

"Wito wangu kwa NMB, malengo yalikuwa kukusanya fedha za fistula kiasi cha Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne, bahati nzuri tumefikia lengo ndani ya miaka miwili, niwasihi endeleeni kutafuta maeneo mengine ya kusaidia kama vile magonjwa ya saratani.

"Mwakani mbio hizi ziwapo na miaka ijayo ziwapo pia, makusanyo yakasaidie changamoto zingine. Pia kuwe na mbio endelevu, kwa ajili ya siyo tu kukusanya fedha za kusaidia matibabu, bali pia liwe jukwaa la mazoezi ambayo ni mhimili wa afya ya kila Mtanzania katika ujenzi wa taifa," aliagiza.

Waziri Mkuu Majaliwa alikiri kuvutiwa na ubunifu huo wa NMB uliozaa Mbio za Hisani za NMB Marathon, huku akizipongeza Kampuni za Bima za Sanlam na UAP kwa udhamini mnono uliowezesha kuvuka lengo la makusanyo ya kusaidia matibabu ya kinamama wenye fistula nchini.

"Shukrani pia kwa wadhamini walioamua kuiunga mkono NMB wakiongozwa na Kampuni ya Sanlam na UAP, ambao wametoa kiasi kikubwa zaidi, Sanlam Sh. milioni 150 na UAP Sh. milioni 100. Kwa kweli Sanlam, UAP na wadhamini wengineo tunawashukuru kama tunavyowashukuru wakimbiaji wote. "Niwasihi wakimbiaji, wadhamini, waandaaji NMB na CCBRT, tuendeleze 'Mwendo wa Upendo,' tusichoke kuchangia, kwani wahenga walisema kutoa ni moyo. Pamoja na jitihada kubwa za serikali katika kuboresha mazingira ya miundombinu ya afya, inahitaji uungwaji mkono na Watazania na wote," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema ukubwa wa tatizo la fistula nchini ambako kuna wagonjwa takriban 10,000, wanaongezeka kwa mwaka wagonjwa 3,000, huku wanaotibiwa wakiwa ni 1,300 pekee, ulisukuma kujitoa kusaidia eneo hilo la jamii.

Alimshukuru Waziri Mkuu Majaliwa kwa kukubali kuwa sehemu ya washiriki tukio hilo lililofanyika chini ya kaulimbiu ya Mwendo wa Upendo ulilenga kurejesha tabasamu usoni mwa kinamama wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu ya fistula yanayofikia takribani Sh. milioni nne.

"Kiasi cha Sh. bilioni moja tulichokusanya katika miaka miwili hii badala ya minne, kinaenda kugharamia matibabu ya fistula kwa zaidi ya wanawake 250 kwenye Hospitali ya CCBRT.

"Wanawake 10,000 wana fistula kote nchini na kuna ongezeko la watu 3,000 kila mwaka, wakati wanaotibiwa ni takribani kinamama 1,300 tu.

"Kwa hiyo tukaona umuhimu wa kuongeza nguvu ya makusanyo ili kusaidia zaidi, kwani Sh. milioni nne ni kiasi kikubwa mno kwa Mtanzania wa kawaida kumudu kugharamia matibabu. "Hii ndiyo siri iliyotusukuma kuona umuhimu wa kuharakisha zaidi kwani wagonjwa wapo wengi na wana uhitaji ambao haupaswi kusubiri miaka minne.

"Leo (Jumamosi) tumekamilisha lengo kwa miaka miwili, tunawashukuru Watanzania waliojitoa kusaidia kulikomboa kundi la kinamama wasiojiweza pale CCBRT," alisisitiza.

Kwa nyakati tofauti, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sanlam, Julius Magabe na Mkurugenzi Mtendaji wa UAP, Donard Muthem aliyewakilishwa na Aulerio Kimario, walisema kwamba afya ya jamii ni miongoni mwa vipaumbele vyao kama taasisi kongwe za bima na kwamba ndiyo siri ya udhamini wao mnono.



Wafanyakazi wa EATV wakifurahia jambo na wafanyakazi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania waliongoozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Bahati Geuzye (wa tatu kushoto), walipotembelea ofisi za EATV Mikocheni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya kukabidhi maboksi ya taulo za kike kwa Meneja Uhusiano wa IPP, Nancy Mwanyika (kushoto), kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wa kike wanaoishi katika mazingira magumu ili kuunga mkono kampeni ya Namthamini inayoendeshwa na EATV. TEA ilichangia katoni 62. **PICHA: EATV**

## Jafo aahidi kuwanyoosha wawekezaji wenye kiburi

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ameahidi kupambana na watu wenye kiburi ambao huwa wanajitapa wamewaweka mfukoni viongozi wa serikali.

Dk. Jafo alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea maeneo ya uchimbaji wa kifusi na kokoto Kigamboni mkoani Dar es Salaam na kukuta uharibifu mkubwa wa mazingira.

Alisema kuna baadhi ya wawekezaji wenye kiburi ambao huwa hawatekelezi maagizo ya serikali kwa madai kwamba hawawezi kufanywa lolote kwa kuwa wamewaweka mfukoni mwao viongozi wa serikali.

Waziri Jafo alisimamisha uchimbaji wa kokoto na kifusi maeneo hayo na kuliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuhakikisha uchimbaji hauendelei hadi wahusika watakapofuata maelekezo.

Alisema baadhi ya wachimbaji wa kokoto na kifusi wameacha mashimo makubwa ambayo yanahatarisha maisha ya binadamu kwa kuwa yamekuwa yakijaa maji wakati wa mvua.

"Nimetoa maelekezo haya, ninataka kuona yanatekelezwa haraka na sitaki kuona watu wenye kiburi maana kuna watu wanajitapa kwamba wanamnunua kila ofisa wa serikali," alisema.

Waziri Jafo alitoa mwezi mmoja kwa NEMC na Manispaa ya Kigamboni kuhakikisha wanasimamia utekelezwaji wa sheria na wakishindwa kufanya hivyo, atarudi na kufunga moja kwa moja shughuli hizo.

"Ninarudia tena sitaki watu wenye kiburi wanaojifanya wako juu ya serikali, unakuta mtu anasema nimenunua maofisa wote wa serikali, nitaendelea na shughuli zangu kama ninavyotaka. Ninataka watu wanaotii sheria, tukienda kiholela holela nchi hii tutaipeleka wapi?

"Mimi ninajua hapa kuna maisha ya watu lakini lazima tuzingatie sheria wakati wa kutafuta riziki. NEMC na Manispaa ya Kigamboni hakikisheni mnasimamia sheria kwa sababu haiwezekani kuchimba na kuacha mashimo," aliagiza.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya mazingira watu wanapochimba kokoto au kifusi, wanapaswa kuhifadhi mazingira hayo kwa kuyafukia ili kuyarejesha katika hali yake ya zamani.

"Nendeni Wazo pale mkaangalie mwenye kiwanda cha Twiga alivyofanya, amechimba malighafi lakini pale alipochimba ameparejesha kwenye mazingira yake ya zamani na panapendeza ninyi mnaacha mashimo mnamwachia nani?" alihoji.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, alisema kuna maeneo mengi ambayo yamekuwa yakichimbwa kokoto na vifusi bila kujali athari za mazingira.

Alisema mbali na kuathiri mazingira maeneo hayo pia yanakuwa hatarishi kwa binadamu kwa kuwa wamekuwa wakiacha mashimo makubwa ambayo yakijaa maji yanaweza kusababisha vifo.

"Tumeshuhudia kwenye eneo moja hapa Kigamboni watu watatu wamepoteza maisha kwa tabia kama hizi za kutojali mazingira. Mimi ninaomba tutekeleze maagizo ya serikali na wataalamu wetu wafuatilie kwa karibu," aliagiza.

Alisema lengo la serikali ni watu wafanye kazi zao kwenye mazingira rafiki ambayo siyo hatari kwa maisha yao na aliwataka wataalamu wa mazingira wawe wanatembelea maeneo hayo mara kwa mara ili kuona kama hayahatarishi maisha.

# Watu 1,200 wapimwa ugonjwa wa moyo Dar

**Na Romana Mallya**

WATU 1,233 wakiwamo watoto wamejitokeza kupima na kupata matibabu ya moyo katika kambi maalum iliyoendeshwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Miongoni mwao wamekutwa na matatizo yanayohitaji kuanza tiba na wengine wanahitaji kufanyiwa upasuaji.

Kambi hiyo ambayo imefanyika kwa ushirikiano wa madaktari wa JKCI na Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC, imebaini watoto 70 wana matatizo ya moyo ya kuzaliwa ambayo ni matundu na mishipa ya damu kutokukaa katika mpangilio wake pamoja na valvu za moyo kuwa na shida.

Kwa mujibu wa taarifa ya JKCI iliyotolewa jana, watu wazima waliofanyiwa vipimo, wamekutwa na matatizo ya shinikizo la juu la damu, kutanuka kwa moyo, kuziba mishipa ya damu na shida ya valvu za moyo.

"Wagonjwa wengine kwa mara ya kwanza wamegundulika kuwa na matatizo ya moyo, ikiwa ni pamoja na kutanuka na kuziba kwa mishipa ya damu ya moyo ambapo asilimia tano tumewapa rufani ya kuja kufanyika vipimo zaidi na kutibiwa katika taasisi yetu," ilisema taarifa hiyo.

Kwa upande wa watoto wenye matatizo, wazazi na walezi wao wameelekezwa kwenda JKCI ili wafanyiwe upasuaji kwenye kambi maalum za upasuaji wa moyo kwa watoto zitakazoanza Oktoba 10, mwaka huu na wengine watahudhuria kliniki kwa ajili matibabu ya ufuatiliaji zaidi.

Kambi hiyo ya kupima na matibabu ya moyo ilifanyika kwa siku tano kuanzia Septemba 26, mwaka huu, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani.

Wananchi walipata fursa ya kupima urefu, uzito, kiwango cha sukari mwilini, kuangalia uwiano wa urefu na uzito, namna moyo unavyofanya kazi, mfumo wa umeme wa moyo pamoja na vipimo vya damu (utendaji kazi wa figo, ini na kiwango cha mafuta kwenye damu).

## TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water
617072202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wetu michuano CAF fungeni hesabu awali

**MWISHONI** mwa wiki hii, Jumamosi na Jumapili wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu kwa upande wa soka, Simba, Yanga, Azam FC na Kipanga ya visiwani Zanzibar, watashuka katika viwanja tofauti kuwania tiketi muhimu kwenye Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa upande wa Simba na Yanga, zitakuwa nyumbani na ugenini kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola na Al Hilal ya Sudan, zikiwania kufuzu hatua ya makundi.

Simba itakuwa ugenini nchini Angola wakati Yanga ikiwa mwenyeji wa Al Hilal kabla ya mechi za marudiano kupigwa Oktoba 16, mwaka huu na timu itakayopata matokeo ya jumla ndiyo itakayofuzu hatua ya makundi na itakayotolewa itaangukia kucheza mechi za mchujo dhidi ya zitakazovuka raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho ili kuwania kucheza hatua ya makundi ya kinyang'anyiro hicho cha pili kwa ubora na utajiri kwa ngazi ya klabu Afrika.

Simba imetinga hatua hiyo kwa kuitoa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwa jumla ya mabao 4-0, ikishinda 2-0 ugenini na kupata ushindi kama huo nyumbani, wakati Yanga ikivuna ushindi mnono wa mabao 9-0 dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini kwa kupata ushindi wa 4-0 mechi ya kwanza na marudiano 5-0, zote zikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa upande wa Azam FC ambayo imeanzia moja kwa moja kwenye raundi ya kwanza, itaanzia ugenini dhidi ya Al-Akhdar Sports Club ya Libya wakati Kipanga FC ambayo itaanzia nyumbani dhidi ya Club Africain ya Tunisia, yenyewe iliitoa Al Hilal Wau ya Sudan Kusini kwa mikwaju ya penalti 4-3 kutokana na matokeo ya bao 1-1 nyumbani na ugenini.

Hivyo, matokeo hayo kwa ujumla yanatupa matumaini makubwa kwa wawakilishi wetu kuweza kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya Afrika na kuzidi kulitangaza soka la Tanzania.

Hata hivyo, ili kutekeleza malengo hayo wachezaji hawana budi kuandaliwa kwa lengo la kuingia uwanjani wakiwa na dhamira moja tu ambayo ni kumaliza mchezo katika mechi ya kwanza ili kuepuka kuwa na mlima mrefu wakati wa marudiano.

Tunatambua ugumu wa michuano hii ya Afrika hususan kwa timu inayocheza nyumbani, hivyo kwa wawakilishi wetu, Yanga na Kipanga FC ambao wataanzia nyumbani, njia rahisi ya kujihakikishia kusonga mbele ni kupata ushindi mkubwa na kuhakikisha hawakubali kuruhusu bao nyumbani.


Katika hilo, hata kwa Simba na Azam FC, zinapaswa kujituma ipasavyo ili kushinda na kama ikishindikana kupata sare, jambo ambalo litarahisisha kazi katika mechi za marudiano wiki ijayo.

Tunaamini wawakilishi wetu wana wachezaji wa kiwango cha juu wakuweza kubadili matokeo uwanjani wakati wowote, hivyo kwa muda huu uliosalia kabla ya mechi hizo ni wakati wakurekebisha makosa madogo waliyoyabaini na kuwajenga wachezaji kisaikolojia ndani na nje ya uwanja.

Sote tunatambua fitina zinazofanywa na timu pinzani katika michuano hii hususan zinapokuwa nyumbani, ambapo hutumia nafasi hiyo kuwavuruga wapinzani wao kisaikolojia, hivyo ni wakati wa kuwandaa wachezaji kisaikolojia ili kuweza kukabiliana na fitina hizo hasa kwa Simba na Azam ambazo zitaanzia ugenini.

Lengo letu ni kutaka kuona zote zikifuzu hatua inayofuata na kuendelea kuipeperusha vema bendera ya nchi kimataifa, hivyo hatuna budi kuwatakia wawakilishi wetu maandalizi mema na mafanikio makubwa katika michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Sababu mashabiki Dar kutokwenda viwanjani

**MENEJA** Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, ameanzisha mjadala wa kwa nini mashabiki wengi wa Dar es Salaam kwa miaka ya hivi karibuni wamekuwa hawaendi viwanjani.

Ila ameanzia mbali kwa kuwataja mashabiki wa timu yake ya Simba kuwa wengi wamekuwa hawana tabia ya kwenda kuangalia mechi ambazo timu yao inacheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Nimefungua mjadala kwa nini watu hawaji uwanjani mechi za Dar. Nimepata majibu mengi, lakini sijaridhishwa nayo na nimeona ya kawaida tu ambayo hayaendani na uhalisia. Nimewasema mashabiki wa klabu yangu ya Simba, wakaniambia eti timu haicheze vizuri msimu huu ndiyo maana, hapana. Kwanza mimi ninavyoona mashabiki hupenda timu yao kwa shida na raha, ndiyo maana utaona kwa wenzetu hata timu inataka kushuka daraja, lakini mashabiki bado wamejazana," alisema Ahmed.

Nimwongezee tu hapo, ni kwamba mashabiki nchi za nje hasa Ulaya, hata timu yao ikicheza mechi ya mwisho tena na timu kubwa wanajazana na wakifungwa mabao, dakika chache kabla mechi kumalizika wanatoa mabango ambayo naona wanakuwa wameyatayarisha kabla ya mechi wakikubali matokeo na kusema wanashukuru, lakini msimu ujao watarejea kwa kishindo, wakiendelea pia kushangilia. Hao ndiyo mashabiki mashujaa wafia timu.

Ahmed akawauliza, mbona hata wakati ule Simba ilipokuwa inacheza soka biriani, ile ya kina Clatous Chama, huku Meddie Kagere, kule Luis Miquissone bado mashabiki wa Simba Dar walionekana kuwa idadi ndogo wanaokwenda viwanjani kuliko hata wa Yanga ambao walikuwa 'tiamaji tiamaji?'

Ni kweli mashabiki wa Simba walionekana kujazana tu Dar pale timu yao ilipokuwa ikicheza mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Ingawa Ahmed ameitaja timu yake na inaonekana ni kama inazidiwa mashabiki na wenzao Yanga, lakini hata hao wanaozidi ni wachache. Kifupi tu ni kwamba mashabiki wa soka Dar hasa wa Klabu za Simba na Yanga uhudhuriaji wao uwanjani umekuwa wa mashaka.

Unaweza kusema sababu ya televisheni, wengi wao wanaangalia huko, lakini mikoani nako zipo, ila huko ndiko timu hizo zinapojaza mashabiki.

Sitaki kwenda mbali sana, nataka nieleze baadhi ya sababu ambazo kama wataalamu watafanya uchunguzi, basi wanaweza kuanzia hapo pia.

Kwanza kabisa tuelezane ukweli ni kwamba mifumo ya kielektroniki irekebishwe na iwe rafiki kwa mashabiki. Pia wengi hawana Ncard. Hapa tu peke yake unaweza kuona kuwa kuna baadhi ya watu wameachwa na wanapata changamoto sana kwenye hili na ndiyo maana utaona hata wanaoingia uwanjani mara nyingi ni wale wale tu. Wengine wakipata changamoto kidogo tu, wanakata tamaa.

Mikoani hakuna changamoto hizo kwa sababu wao nao wana mifumo yao ya kuingia.

Kingine ni kwamba mashabiki wa soka wanachukuliwa kama watu wanaokwenda kudowea chakula cha watu kwenye shughuli na si wateja.

Mara nyingi hawachukuliwi kama wateja, ndiyo maana wanaanza kukutana na changamoto tangu mlangoni, kuingia, hakuna mifumo rafiki ya kuingia, unaweza kudhani mtu anaingia gerezani. Hadi anaingia yupo hoi na amenusurika virungu, kuumwa na mbwa, kufukuzwa huku na huko.

Wanapokaa tatizo, usalama wao mdogo, na hata vyoo pia changamoto, kutoka nako ni tabu, unaweza kukuta geti moja tu limefunguliwa.

Mikoani wanaweza kuvumilia kwa sababu ya kuziona klabu hizo na wachezaji wake ni nadra sana, ndiyo maana wanajaa, lakini wa Dar es Salaam hawawezi kuvumilia hilo.

Huwa tunaona mashabiki wanapigwa mitama na maaskari, virungu, hii yote inasababisha mashabiki hasa Dar kuamua kubaki majumbani na kuangalia kwenye vibanda umiza au kwenye mabaa.

Usalama wa mashabiki mara tu wanapotoka viwanjani Dar nao ni mdogo na mara nyingi kumeripotiwa uporaji mita chache tu kutoka Uwanja wa Benjamin Mkapa, iweje kipindi hiki ambacho kumeripotiwa kuwa na Panya Road sehemu mbalimbali?

Kwa sasa asilimia 90 za mechi za Dar zinachezwa usiku, mji kwa sasa umepanuka sana, kuna watu wanaishi Boko, Kisemvule, Goba, Chanika na sehemu nyingi ambazo ni nje ya mji na wakifika huko, wanaingia tena ndani zaidi kwa usafiri wa bodaboda kwa gharama kubwa, lakini unaweza kukuta sehemu zingine kwa muda huo usiku hakuna usafiri tena, hivyo kuwaogopesha wengi kwenda viwanjani. Nadhani kuna baadhi ya mechi za ligi ziendelee kuchezwa jioni Benjamin Mkapa.

Sababu hizo, zingine na kuendelea kutowafanya Watazamaji kama wateja, pamoja na ndani ya uwanja kutokuwa na huduma zozote za kijamii ambazo zinaweza kuwavutia mashabiki, zinasababisha mashabiki wa soka kupungua. Mjadala uendelee na uchunguzi ufanyike ili kujua sababu zingine zaidi ziunganishwe na hizi chache nilizoziainisha ili ufumbuzi upatikane kwani gharama kubwa zinatumika kuziendesha timu na uhudhuriaji viwanjani kwa wingi ni sehemu kubwa ya mapato.

## HABARI KITAIFA




Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga (wa pili kulia), akimkabidhi cheti cha ushiriki Dk. Winland Samwel wa Hospitali ya Rufani Maweni, Kigoma, katika kilele cha mafunzo ya tathmini za ulemavu uliosababishwa na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi yaliyoandaliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Madaktari waliohudhuria walitoka mikoa ya Kigoma, Tabora, Singida na Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TFRA yataka Ma-DC, Ma-RC kudhibiti utoroshwaji mbolea

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imewataka wakuu wa mikoa kudhibiti utoroshaji wa mbolea ya ruzuku mipakani na wahakikishe inauzwa kwa walengwa nchini.

Vilevile, mamlaka hiyo inatarajia kuwasajili wakulima milioni saba kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku na mwisho wa usajili ni Desemba mwaka huu.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa viongozi hao, Mkurugenzi wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, alisema mbolea ya ruzuku inatakiwa kuwafikia wakulima ili kutumika kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

"Tunaomba wakuu wa mikoa mtusaidie suala la utoroshaji wa mbolea ya ruzuku katika mipaka ambayo inapitishwa," alisema Dk. Ngailo.

Akizungumzia kuhusu kusajili wakulima Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wanatarajia kusajili wakulima milioni saba kwa ajili ya upataji wa mbolea ya ruzuku.

Bashe alisema usajili kwa wakulima umepangwa kufikia ukingoni Desemba mwaka huu katika mikoa mbalimbali.

Alisema kuna mikoa ambayo usajili wa wakulima unasuasua, akiwataka wakuu wa mikoa kuhakikisha wanahimiza maofisa ugani kutoa elimu kwa wakulima ya umuhimu wa kujisajili kwa ajili ya upatikanaji wa mbolea ya ruzuku.

Alisema mpaka sasa tayari wameshajili wakulima milioni 1.2 na kuongeza kuwa wakuu wa mikoa wahitahitaji kuhimiza suala la usajili katika mikoa wanayotoka.

Kuhusu ujenzi wa maghala, Bashe alisema yatajengwa katika mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kuhifadhi mazao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema ruzuku ya mbolea ni dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia wakulima ili wazalishe kwa tija kwa maslahi yao mwenyewe na taifa kwa ujumla.



Alisema: "Rais Samia Suluhu Hassan ametoa ruzuku hii kwa wakulima ili kuwasaidia lakini tunaona nchi zingine zikiwaacha wakulima wanapambana na hali zao lakini Rais Samia akasema hapana lazima niwasaidie wakulima wangu," alisema.

## SBL, FDH watoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kushirikiana na Shirika la Foundation of Disabilities Hope (FDH) wamedhamini mafunzo ya siku mbili ya kujiongezea kipato kupitia kilimo kwa watu wenye ulemavu ili kuchochea ukuaji uchumi shirikishi nchini.

Mafunzo hayo ambayo yalifanyika mwishoni mwa wiki mjini Dodoma, yalishirikisha zaidi ya watu 100 wenye ulemavu waliopata mafunzo ya kilimo biashara, ujasiriamali na ujuzi wa masuala ya fedha ili kuwasaidia kuingiza kipato zaidi katika shughuli zao za kila siku za kiuchumi.

Akizungumzia mafunzo hayo jana, Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya dhamira yao ya kukuza kasi ya uchumi nchini na kudumisha mpango wao wa miaka 10 wa kujenga jamii shirikishi na endelevu.

"Tunajivunia kushirikiana na FDH kuwezesha mafunzo haya ya kuwasaidia watu wenye ulemavu kuongeza mapato yao ambapo zaidi ya watu 100 watanufaika na fursa hii.

"Tuna imani tutaweza kutengeneza kundi jipya la maofisa kilimo na wataalamu wa kilimo biashara na hivyo kuimarisha sekta yetu ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu.

"Pia tunatazamia kutoka kundi hili kununua malighafi yetu ya utengenezaji bia ambayo hatimaye itainua kipato chao na kuinua kiwango chao cha maisha," alisema.

Wanyancha alisema SBL imejitolea kushawishi wadau wengine nchini kuunga mkono jitihada za kujenga jumuiya jumuishi ambapo kila mtu, bila kujali hali yake ya kimwili, anaweza kufurahia maisha popote na wakati wowote.


Alisema: "Tuko tayari kufanya kazi na taasisi za watu wenye ulemavu katika kila idara ili kuhakikisha tunajenga jamii uendelevu na kusaidia serikali kufikia ukuaji wa uchumi jumuishi bila kumwacha mtu yeyote nyuma," alisema.

Naibu Waziri wa Kilimo, Athony Mavunde na Mbunge wa Dodoma Mjini, alisema anatambua kazi inayofanywa na SBL katika kusaidia kilimo nchini kupitia shughuli zake za biashara ambazo kwa wastani wananunua zaidi ya tani 18,000 za nafaka kwa mwaka kutoka kwa wakulima.

"Tunaishukuru sana SBL kwa kuleta ustahimilivu wa kilimo katika nchi yetu kwa kujumuisha watu wenye ulemavu. Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, tangu aingie madarakani ameonyesha nia ya dhati ya kufanya kazi na sekta binafsi kama injini ya kukuza uchumi, hasa katika kilimo.

"Ndiyo maana tunajitahidi kuifanya sekta hii kuwa ya kibiashara kwa kuwavutia wawekezaji na wakulima wengi zaidi ambao wataleta mapinduzi katika sekta hii na kuchochea ukuaji wa uchumi. Na kwa hili, tunaipongeza SBL kwa kuunga mkono wito wetu," alisema.

## KABWELA



# Waziri: GGML ni mfano bora Afrika kutoa huduma za jamii

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Madini, Dk. Dotto Biteko amesema Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Dhahabu Geita (GGML) ndiyo kampuni ya uchimbaji inayoongoza Tanzania na Afrika kwa ujumla kwa kutekeleza kikamilifu Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR).

Pia amesema wizara hiyo inajipanga kutengeneza kanuni na mwongozo maalum ambao utafanya watu wote watekeleze miradi ya CSR bila kutegea.

Dk. Biteko alitoa pongezi hizo jana alipotembelea mgodi wa GGML ili kushuhudia miradi mipya ya uchimbaji dhahabu inayofanyika katika mgodi huo mkoani Geita.

Alisema kwa muda mrefu GGML wamekuwa wakitekeleza kwa kiwango cha kuridhisha mpango huo wa CSR na mtu yeyote atakayesema mgodi huo haufanyi vizuri kwenye CSR, atakuwa anawaonea.

"Mimi ningependa tuwe wakweli, nchi hii kampuni inayofanya vizuri kwenye CSR kwenye madini ya kwanza ni GGM. Wamefanya kazi nzuri," alisisitiza Dk. Biteko.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo imekuwa ikishirikiana na wananchi katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa jamii inayozunguka migodi, hususani katika ujenzi wa hospitali, shule na vifaa vya tiba ili jamii ipate huduma bora.

Alisema ziara yake ililenga kuona hali ya mgodi baada ya kuhama kutoka kwenye uchimbaji wa shimo la wazi kwenda kwenye uchimbaji wa chini kwa chini.

"Hofu yetu ilikuwa ni kwamba kwa kuwa mgodi huu utakuwa kwenye hatua ya uendelezaji, tulidhani utashuka lakini sasa tunafurahi kwamba mgodi wamejitahidi kuweka uzalishaji kuwa kwenye kiwango kinachotakiwa," alisema.

Makamu Rais wa AngloGoldAshanti anayeshughulikia maendeleo kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, alisema kampuni hiyo inaendelea kushirikiana na wananchi ili kujenga uhusiano mzuri katika mazingira yote yanayozunguka mgodi.

Pia alimshukuru Dk. Biteko kwa kutambua jitihada zao kwa namna kampuni hiyo inavyonunua bidhaa na kutumia huduma za kitanzania. "Mtafahamu kwamba mgodi huu umekuwa wa uchimbaji wa wazi tangu kwa miaka 15, kuanzia mwaka 2002 hadi 2015... kuanzia mwaka 2015 tumeanza kuhamia chini kwa chini, kufikia leo tuna miradi mitatu mikubwa, mradi wa Star and Commet, Nyankanga na Geita Hill ambayo yote inazalisha. Pia miradi hii inasaidiana na miradi ya wazi ya Nyamlilima," alisema.

Aliongeza kuwa asilimia kubwa ya bidhaa za mgodi huo sasa karibu asilimia 70 ya fedha inayotumiwa na GGML inanunua bidhaa kutoka Tanzania.

Shayo alisema lengo la GGML ni kuhakikisha inaendelea kuwa kinara kwa kufanya vizuri ili watu wavutiwe kuwa mwajiriwa wa GGML na wote wanaozunguka mgodi huo kuwa na ujirani wa manufaa.

Mbunge wa Geita Mjini, Costantine Kanyasu (CCM) aliipongeza GGML kwa kushirikisha kikamilifu wazawa wa Geita na Watanzania kwa ujumla katika utoaji wa huduma mbalimbali ndani ya mgodi.

Alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa zinazotangazwa na GGML ili kupata zabuni za kutoa huduma ndani ya mgodi huo.

"Sisi Halmashauri ya Mji wa Geita ni wafaidika namba moja kwa sababu katika taarifa kwenye CSR inayotengwa tunapata asilimia 54 ya Sh. bilioni tisa ambazo tumezielekeza kwenye maeneo manne makubwa.

"Maeneo haya ni kwenye elimu, miundombinu afya, miundombinu ya kawaida ya kijamii kama viwanja vya mpira, lakini sasa tunakwenda kwenye uchumi wa mtu mmoja mmoja... hakika tunaendelea vizuri," alisema.



Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko (kushoto), akipata maelezo kwa Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Stephen Mhando, namna kampuni hiyo inavyotekeleza kikamilifu Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR), wakati wa Maonesho ya Tano ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini katika Viwanja vya Bombambili mkoani Geita jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yakusanya maoni kuboresha Sera ya Vijana

**Na Golden Kisapile, (TUDARCo)**

SERIKALI imeanza kukusanya maoni ya uboreshaji wa Sera ya Vijana ya Mwaka 2007 ili kuwa na nyaraka zinazokidhi matakwa na mahitaji ya sasa kwa kundi hilo.

Ofisa Mwandamizi wa Maendeleo ya Vijana Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana na Wenye Ulemavu, Amina Sanga, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kikao cha vijana jijini Dar es Salaam.

"Tunafanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Vijana ya Mwaka 2007 ambayo imetumika kwa miaka mingi, ili twende kuandaa sera nyingine, inabidi tufanye tathmini na kuangalia nini kinastahili kubadilishwa au kuboreshwa.

"Tathmini hiyo haiwezi kufanyika bila kurudi kwa vijana wenyewe kuwauliza utekelezaji wa sera iliyopita wameonaje kwa sababu sera iliyopita ilikuwa na mambo 29 kama vile ya afya kwa vijana, ajira kwa vijana.

"Kila kipengele cha vijana wamepewa nafasi ya kusema nini kimefanyika na nini wanataka kifanyike. Kwa mfano, kwenye eneo la afya, teknolojia, mikopo, ushiriki na ushirikishwaji kwa vijana na wameonaje kwenye utekelezaji wa ile sera ya mwaka 2007?" Sanga alifafanua.

Alisema mwamko wa vijana ni mkubwa, akibainisha kuwa wengi wamejitokeza kutoa maoni huku akiwataka wengine kuendelea kufanya hivyo kupitia maeneo mbalimbali.

Kijana Aisha Omari alisema: "Nimekuja kushiriki kwenye jambo hili ili kujua upungufu wa Sera ya Vijana ya Mwaka 2007, nitatoa maoni yangu ya uundwaji wa sera mpya, ninawasihi wenzangu wajitokeze watumie vyema mitandao yao ya kijamii kupaza sauti zao."

# TLP yataka wanachama wake wasifukue makaburi

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha TLP kimewataka wanachama wake kusahau yaliyopita badala yake waweke mikakati ya kukiimarisha kwa kuwa kuibua yaliyopita ni sawa na kufukua makaburi.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo, alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam wakati wa kikao kilichowakutanisha viongozi wa TLP wa mkoa huo Makao Makuu, Magomeni Usalama.

Kikao hicho kililenga kuweka mikakati ya kukifufua chama hicho, aliyekuwa Mwenyekiti wa TLP Taifa, Amos Kalumira akisema mwenyetiki wa chama hicho taifa, marehemu Agustine Mrema kumpigia debe mgombea urais wa CCM wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, kuliwatia dosari, hivyo hajui wapi wataanzia kurudi kwenye mstari.

"Tunashindwa tuanzie wapi kushawishi Watanzania na baadhi ya wanachama waliokata tamaa, kwani kwa kitendo kile cha mwenyekiti wetu kumpigia debe mgombea huyo, chama kilionekana ni sehemu ya CCM," alisema Kalumira.

Hata hivyo, Katibu Mkuu alisimama na kumwomba aachane na yaliyopita, badala yake viongozi wa TLP Mkoa wa Dar es Salaam wajadili mbinu zitakazokisaidia chama hicho kukubalika.

"Ninaomba tuachane na mambo hayo, kwani wote hawapo tena katika dunia hii, tukisema tujadili itakuwa ni sawa na kufukua makaburi, sisi tunataka kujenga upya chama chetu, yaliyopita tuachane nayo," alisema Lyimo.

Alisema TLP ya sasa siyo ile ya zamani huku akithibitisha kuwa wapo baadhi ya wanachama waliokerwa na uongozi uliopita na kuongeza kuwa sasa wameamua kujipanga upya, hivyo hawana budi kuachana na yaliyopita.

Kauli hiyo ya Katibu Mkuu iliungwa mkono na Mwenyekiti wa Wazee wa TLP Taifa, Consolata Momba, aliyewataka wanachama kuwa kitu kimoja kwa lengo la kukiimarisha chama chao.

"Tumeamua kujipanga upya, tuelekeze nguvu zetu huko, tufukue makaburi kwani hayatusaidii kitu, badala yake kila kiongozi kwenye eneo lake akutane na wanachama na kujadili njia ya kurudisha uhai wa TLP," alisema Consolata.

Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Alhaj Omary Mkadam, alisema kikao hicho ni mwanzo wa vikao vingine vitakavyofanyika kila mkoa Tanzania Bara na visiwani kwa lengo moja la kurejesha uhai wa TLP.

"Viongozi wa kitaifa tutazunguka mikoa ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa ajili ya kuitisha vikao na kuweka mikakati ambayo itasaidia kurejesha uhai wa chama kabla ya uchaguzi wa mwaka 2024/2025,"alisema Alhaji Mkadam.

Alhaji Mkadam alisema chini ya uongozi wake hawataki kuona chama kinaedelea kuwa kama cha mfukoni kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, badala yake atajitahidi kushirikiana na viongozi wenzake kukifufua.

"TLP ni chama kikubwa na ni miongoni mwa vyama vyenye usajili wa kudumu, hivyo sisi kama viongozi hatuna budi kuhakikisha kinafanya shughuli za kisiasa na siyo kuendelea kuwa kama hakipo," alisema.

# ACT yataka hatua kumaliza migogoro wakulima, wafugaji

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuchukua hatua za muda mfupi, kati na mrefu kukabiliana na migogoro ya wakulima na wafugani nchini.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu alitaka kuchukuliwa kwa hatua hizo alipozungumza na wanachama wa chama hicho katika Kata ya Mchoteka wilayani Tunduru jana.

"Hivi karibuni nilifanya ziara mkoani Lindi. Karibu kila kata niliyokwenda hasa Wilaya ya Kilwa, nilikuta visa vya mapigano ya wakulima na wafugaji ambayo watu wengi wamejeruhiwa na hata kuuawa.

"Hali hiyo ilinitisha sana, nikaomba kuonana na Waziri Mkuu. Ninashukuru alinikubalia tukakaa chini na kuzungumza. Nilimweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kama hatua za upesi hazitochuliwa, mapigano yatasambaa maeneo mengi na kuhatarisha usalama nchini," alisema.

Ado aliendelea: "Nimefika hapa Tunduru, ninaona tatizo hili pia limekita mizizi. Migogoro ya wakulima na wafugaji imekuwa janga la kitaifa linalohitaji hatua za muda mfupi, kati na mrefu.

"Tunahitaji mipango bora ya matumizi ya ardhi inayopangwa na kusimamiwa vizuri. Tunduru hatuna tatizo la ardhi. Ukubwa wa Tunduru ni zaidi ya Mkoa wote wa Mtwara.

"Muhimu wafugaji wadhibitiwe wasiingie wilayani kiholela na wale wanaoruhusiwa watengewe maeneo yao kuepuka mwingiliano na wakulima. Viongozi wa Serikali pia wasimame imara kuwadhibiti wafugaji wanaovamia mashamba na vijiji vya wakulima."

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu huyo amewaeleza wanachama na viongozi wa ACT-Wazalendo kujiandaa mapema kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025 kwa vile chama chao kwa kushirikiana na wadau wengine wa demokrasia wanapambana kuhakikisha uchaguzi huo unakuwa za huru, haki na kuaminika.



Dereva wa bodaboda, Onesmo Ndarusanze, akitoa elimu ya kujikinga na rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Salma Kikwete, Kijitonyama Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, katika mwendelezo wa kampeni ya Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana, inayoendeshwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mradi wa gesi ya LNG kukamilika Desemba

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na washirika wake Norway kuhakikisha majadiliano ya msingi kuhusu mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia nchini (LNG) yanakamilika ifikapo Desemba mwaka huu.

January aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, aliposhiriki warsha ya viongozi iliyofanyika katika kampuni ya Equinor, unakotekelezwa mradi huo mji wa Hammerfest, Kaskazini mwa Norway.

Katika warsha hiyo, Waziri January na viongozi wengine kutoka Tanzania walijadili maandalizi ya mradi huo wenye thamani ya Sh. trilioni 70 utakaotekelezwa mkoani Lindi.

Viongozi wengine walioshiriki warsha hiyo ni Balozi wa Tanzania Nordic, Grace Olotu, Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali. Viongozi hao pia walikutana na wafanyabiashara wa eneo hilo wanaonufaika kwa kutoa huduma kwenye eneo hilo la mradi wa Equinor na Watanzania wanaofanya kazi katika mradi huo.

Mtambo uliojengwa kwenye mradi huo wa Equinor huchakata Sh. bilioni 4.6 za mita za ujazo za gesi asilia kwa mwaka pamoja na bidhaa zingine kama gesi ya kupikia (LPG).

## Chifu Mwakatumbula akabidhiwa Ikulu yake

**Na Mwandishi Wetu,** RUNGWE

KATIKA kutekeleza adhima ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni kiongozi wa machifu nchini, kuuhuisha kuendeleza tamaduni za kichifu nchini, Chifu wa Kabila la Wanyakyusa, Chifu Edwin Mwakatumbula amekabidhiwa Ikulu yake ya kichifu na kiongozi wa machifu wadogo wa kabila hilo.

Akizungumza katika tukio hilo la kihistoria jana, Chifu Mwakatumbula alisema imekuwa siku ya baraka kwenye himaya hiyo na kwake kukabidhiwa Ikulu hiyo iliyojengwa mwaka 1900.

Alisema kuwa kazi aliyokabidhiwa na machifu wadogo wa kabila hilo ataendelea kuifanya kwa kuzingatia mila na desturi za kabila hilo maarufu nchini.

Kiongozi huyo wa kimila alisema kuwa aliporithi uchifu wa kabila hilo kutoka kwa marehemu Chifu Daudi Mwakatumbula miaka 10 iliyopita, amejitahidi kuendeleza mila za kabila hilo huku akidumisha amani, umoja na mshikamano miongoni mwa Wanyakyusa wote nchini.

Chifu Mwakatumbula alisema jamii ya Wanyakyusa nchini inapaswa kujivunia amani na umoja miongoni mwao huku akiahidi kuendela kulilea kabila hilo kwa kuzingatia misingi na tamaduni zao.

Mbali ya kuwa Chifu, kiongozi huyo ana historia kubwa kwenye siasa za Tanzania, akitoa huduma kwenye nafasi mbalimbali za uongozi na kiutawala kwenye maeneo mbalimbali nchini ambapo kwa nyakati tofauti amekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya wilaya ambapo mara ya mwisho alikuwa katibu wa chama Wilaya ya Geita.

Chifu huyo ni miongoni mwa watoto 129 wa marehemu Chifu Bentamanile Mwakatumbula wa kabila hilo ambaye alifariki dunia mwaka 1955, akiacha wake 52.

Vitabu vya kihistoria vya kabila la Wanyakyusa vinamtambua Chifu Bentamanile Mwakatumbula kwa mageuzi makubwa ya kiutawala aliyoyafanya wakati wa utawala wake wa miaka 45.

Katika kuthibitisha hilo, alikuwa chifu pekee kutoka Tanganyika aliyekabidhiwa cheti cha heshima kutoka kwa Malkia Elizabeth II wa Uingereza.

Wakati wa utawala wake, alihesabiwa miongoni mwa machifu wa kimila waliokuwa mstari wa mbele kupambania uhuru wa nchi huku Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere akisema kuwa kazi kubwa waliyoifanya kipindi hicho katika mikoa ya nyanda za juu kusini hususan Mkoa wa Mbeya zilikuwa za kutukuka na kurahisisha kuiunganisha nchi.

# Walalama kutumia maji yasiyo salama

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI wa Buyuni, Kata ya Pembamnazi wilayani Kigamboni mkoani Dar es Salaam wameiomba serikali kuharakisha ujenzi wa bomba la kuvuta majisafi ili waondokane na shida ya maji wanayopitia kwa sasa.

Katika mazungumzo yao na Nipashe mwishoni mwa wiki, wakazi hao walisema maji wanayotumia siyo salama kwa afya zao na wana hofu ya kupata mlipuko wa magonjwa kutokana na visima wanakochota maji kuwa wazi.

Amina Selemani, mkazi wa eneo hilo, alisema kutokana na shida hiyo wanalazimika kuchota maji kwenye visima vya chemchem kwa ajili ya kufulia ambavyo maji yake ni machafu, hali inayosababisha wakati mwingine kupata maradhi ya ngozi.

"Hayo maji ya kisima tunayatumia kwa shida tu, lakini yanatusababishia maradhi ya ngozi. Wakati mwingine unavaa nguo unaanza kuwashwa, hii yote ni kwa sababu maji yale yapo wazi yanaingia kila namna ya taka, pia wakati wa jua kali visima hivyo vinakauka," alisema. Mwajabu Mohamed, mkazi mwingine wa eneo hilo, alilalamika kuwa analazimika kutumia Sh. 1,500 kwa siku kununua madumu matano ya maji ya kisima yenye chumvi kwa ajili ya kupikia na kuosha vyombo, ambapo dumu la lita 20 linauzwa Sh. 300 huku la maji ya bomba yanayofaa kunywa Sh. 500.

"Kwa kweli kwa maisha yangu mimi ninayetegemea shughuli za uvuvi kutoa Sh. 2,000 kila siku ni gharama sana.

"Kwa siku gawiwo langu la samaki ni Sh. 5,000, sasa nikitoa hapo ninabakiwa na Sh. 3,000 haitoshi kuhudumia familia, lakini nitafanyaje, maji nayo ni muhimu? Serikali ituangalie kwa hili," alisema.

Fatuma Mwalimu alisema anashindwa kufanya shughuli nyingine za maendeleo kwa ufasaha kwa sababu anatumia zaidi ya saa tatu kusaka maji ya kupikia kwa kuwa foleni ni kubwa, pia viungo vya mwili vinauma kutokana na kubeba madumu ya maji.

Mama huyo mwenye familia ya watoto saba, alisema siku anayokwenda kuchota maji analazimika kusimamisha shughuli ya kutengeneza viatu na kofia ambazo anazitegemea kumwingizia kipato.

"Tatizo lilipo kwenye maji ya kupikia na kunywa foleni ni kubwa na inasababishwa na hawa wenye madumu kwa ajili ya kuuza.

"Ukienda kuchota maji ujue kabisa shughuli zako nyingine zinasimama, lakini kwa vile fedha ya kununua kwenye madumu sina inabidi nikubaliane na vyote," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Shaban Shaha, alisema wanapitia kadhia hiyo kwa kuwa mabomba mengi yamepasuliwa na wakulima.

Alisema wamewasiliana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) ambao walifanya ukaguzi mwezi uliopita na kuahidi kufunga mabomba kwenye visima ili maji yasambazwe kwenye nyumba za watu.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, walifanya juhudi kutafuta wafadhili ili wawachimbie visima virefu na walifanikiwa kupata mmoja aliyewachimbia kisima katika soko la samaki Buyuni na Kwazozo ambako wananchi wanachota maji bila malipo.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (wa tatu kushoto), akifurahia pamoja na Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal (wa pili kushoto), Mkuu wa Shule ya Msingi Mkoani, Mwalimu Almasi (kushoto) na wanachama wa klabu hiyo, baada ya makabidhiano ya madawati 100 kwa Shule ya Msingi Mkoani jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Klabu ya Rotary imeshatoa madawati zaidi ya 1,500 kwa shule mbalimbali yenye thamani zaidi ya Sh. milioni 240. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rotary yakabidhi madawati 100 Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Rotary ya Dar es Salaam imekabidhi madawati 100 kwa ajili ya Shule ya Msingi Mkoani, Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam ili kuwasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu kwenye mzingira mazuri.

Madawati hayo ni kati ya zaidi ya 1,500 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 240 yaliyotolewa na klabu hiyo kwa shule mbalimbali nchini.

Madawati hayo yalipokewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, mwishoni mwa wiki katika shule hiyo iliyopo Ilala Boma.

Rais wa klabu hiyo, Nikki Aggarwal alisema wamekuwa wakishirikiana na jamii kuboresha huduma za jamii na wamekuwa wakisaidia sekta ya elimu kwa kuchangia madawati.

Alisema wanaendelea na mradi wa kutoa madawati unaokwenda sambamba na upandaji miti ili kuhifadhi mazingira.

"Hivi sasa mradi wetu huu umeshatoa madawati zaidi ya 1,500 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 240 kwa shule mbalimbali. Kwa hakika huu ni mchango mkubwa na tunaendelea nao," alisema.

Kiongozo hiyo alisema moja ya malighafi kwenye kutengeneza madawati ni mbao na ndiyo sababu mradi wao huo unakwenda sambamba na upandaji wa miti ili kutunza mazingira.

Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea madawati hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija alisema mchango huo ni muhimu kwa kuwa serikali inafanya jitihada kuimarisha elimu, hivyo mchango wa wadau kama Rotary ni muhimu ili kuharakisha maendeleo katika sekta ya elimu.

Alisema serikali inathamini ushirikiano unaoonyeshwa na taasisi kama Rotary na akaitaka klabu hiyo kuendelea kushirikiana na serikali na serikali itatoa kila aina ya ushirikiano unaotakiwa katika miradi ya kijamii inayofadhiliwa na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mkuu wa Shule ya Mkoani, Mwalimu Almasi aliishukuru Rotary kwa msaada huo utakaopunguza tatizo la uhaba wa madawati, akisema kuwa madawati hayo yatumiwa na wanafunzi 300 kwa wakati mmoja.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza dawati moja katika shule za msingi kutumiwa na wanafunzi watatu.

Ripoti ya Mdhibiti na Ukaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu, mbali na mambo mengine, inabainisha kuwapo uhaba mkubwa wa miundombinu na samani katika shule za msingi na sekondari, akiitaka serikali ichukue hatua kutatua shida hiyo.

# Tanzania kunufaika mabilioni ya Japan

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA ni moja ya nchi za Afrika zitakazonufaika na fedha za Mfuko wa Kukuza Uwekezaji barani Afrika kutoka Serikali ya Japan zitakazotolewa kuanzia Machi mwakani.

Mwenyekiti wa Timu ya Afrika ya KEIZAI DOYUKAI (Japan Association of Corporate Executives), Mutsuo Iwai, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ofisini kwao, Marunouchi, Chiyoda-ku jijini Tokyo, Japan.

"Ifikapo Desemba mwaka huu, tutazindua kampuni ya kusimamia mfuko huu wa uwekezaji wenye manufaa barani Afrika na utekelezaji utaanza Machi, 2023. Tunataraji ifikapo Machi, 2024 tutakuwa tumetoa Dola za Marekani milioni 100 kwa kampuni za vijana wanaochipukia ili kuwajengea ubia, kujifunza teknolojia mpya na kubadilishana ujuzi," alisema.

Alisema fedha hizo za uwekezaji kwenye mitaji ya kuanzisha biashara (start-ups) zimelenga kukuza biashara ambazo zitatatua kero za kijamii zikiwamo sekta za afya, kilimo, nishati na kuimarisha uhifadhi wa mazingira.

Utolewaji wa fedha hizo ni utekelezaji wa ahadi ya Waziri Mkuu wa Japan, Fumio Kishida aliyoitoa Agosti 27, mwaka jana, kwenye Mkutano wa Nane wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaohusu Maendeleo ya Japan na Afrika (TICAD 8) uliofanyika Tunis, Tunisia.

Kishida alisema Japan imelenga kukuza uwekezaji ambapo safari hii wamelenga kuwainua vijana wanaoanzisha makampuni kwani hatua hiyo itawapa fursa vijana wa Afrika na wa Japan kufanya kazi kwa karibu.

KEIZAI DOYUKAI ni taasisi binafsi iliyoanzishwa Aprili 30, 1946 yenye wanachama 1,500 ambao ni watendaji wakuu na wamiliki wa kampuni kubwa za Japan wanaojihusisha na utoaji suluhisho kwa masuala ya kisera yanayohusu maendeleo ya nchi yao na dunia kwa ujumla.

Waziri Mkuu pia alikutana na wawakilishi wa Shirikisho la Wafanyabiashara wa Japan (KEIDANREN) ofisini kwao Otemachi, Chiyoda-ku, jijini Tokyo, ambako Mwenyekiti wa Kamati ya nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Hajime Kawamura, alimweleza shirikisho lao linavyojihusisha na miradi ya maji, barabara, nishati, mawasiliano utengenezaji wa kemikali na ununuzi wa mazao.

Wawakilishi wa kamati hiyo wanaotoka kampuni za Sumitomo, Marubeni, Toshiba, Komatsu na Mitsubishi walimweleza Waziri Mkuu nia yao ya kuwekeza kwenye miradi ya nishati ikiwamo uzalishaji wa umeme kwa kutumia jotoardhi, usambazaji wa umeme, usambazaji wa gesi (LPG), huduma za mawasiliano na TEHAMA.

KEIDANREN (Japan Business Federation) jumuiya ya kiuchumi iliyoanzishwa Agosti 16, 1946 yenye wanachama 1,494 ambao ni wawakilishi wa kampuni za Kijapan, ina vyama 108 vya wenye viwanda na taasisi 47 za kiuchumi kutoka mikoa yote.

Waziri Mkuu aliwaeleza wafanyabiashara wa makundi yote mawili kwamba serikali iko tayari kufanya kazi na wawekezaji na ndiyo maana iliamua kuboresha miundombinu ili kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu.

"Utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, utulivu na amani vilivyoko nchini, hali nzuri ya hewa, ujenzi wa bandari, reli na barabara, umeme na maji unawahakikishia wawekezaji uhakika wa mitaji pindi mnapoamua kuwekeza nchini Tanzania," alisema.

Waziri Mkuu aliwahamasisha waje nchini kuwekeza kwenye sekta ya utalii ikiwamo ujenzi wa hoteli za nyota tano na kuanzisha michezo ya majini kwenye fukwe za bahari Zanzibar na Bara.

"Pia angalieni uwezekano wa kuwekeza kwenye kilimo cha mashamba makubwa na ujenzi wa viwanda. Lengo la serikali hii ni kuendelea kukuza uchumi kupitia sekta mbalimbali ikiwamo viwanda," alisema.





## Watanzania washauriwa kusitisha safari za Uganda

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

RAIS wa Chama cha Madaktari nchini (MAT), Dk. Shadrack Mwaibambe, amewasihi Watanzania kusitisha safari zisizo na ulazima kwenda Uganda, ambako kuna mlipuko wa ugonjwa wa ebola.

Alitoa ushauri huo juzi jijini Arusha, wakati wa mkutano wa 54 wa chama hicho.

Mwaibambe alisema: "Kumekuwapo na mwingiliano mkubwa sana wa wananchi kwenda nchi jirani, kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Uganda hapo siyo mbali ni kilometa 200 kutoka mpaka wa Tanzania, hivyo ni lazima kila mmoja wetu atoe elimu ya kutosha ili wananchi waweze kuchukua tahadhari mapema,"alisema.

Alisema kutokana na kuwapo kwa mlipuko huo, jamii inatakiwa kuelimishwa mapema kuchukua tahadhari ikiwamo kuepukana na safari zisizo za lazima kwenda nchini Uganda.

Dk. Mwaibambe, alisema kuwa kutokana na kuripotiwa kwa ugonjwa huo Uganda, ni muhimu serikali ikachukua tahadhari mapema ili ugonjwa huo usiingie nchini.

Alisema: "Kutokana na ugonjwa huo, ni vizuri tahadhari ikachukuliwa kwenye viwanja vya ndege, kwa kuwakagua watu wanaoingia na watakaogundulika kuwa na ugonjwa huo wawekwe karantini."

Mtaalamu wa Afya ya Kinywa na Meno wa Mkoa wa Arusha, Dk. Omar Chande, alisema ni vizuri MAT kikaongeza nguvu zaidi katika kuhamasisha utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwenye vituo vya afya ili watu wote wapate mhamko wa chanjo hiyo.

Aidha, aliwashauri wadau mbalimbali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya kuchukua tahadhari kuhusu ugonjwa huo ili usiweze kuingia huku nchini.

# Siasa za ukanda, ukabila zamchefua naibu waziri

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, amesikitishwa na siasa za ukanda, rika na ukabila zinazoendelea ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Longido mkoani Arusha, akidai kuwa hali hiyo imesababisha mgawanyiko wa wananchi wa eneo hilo.

Dk. Kiruswa ambaye ni Mbunge wa Longido, aliyasema hayo juzi wakati wa uchaguzi wa Mwenyekiti wa Wilaya hiyo na nafasi nyingine muhimu za kichama.

Kutokana na athari anazodai kuziona zitajitokeza na kuiathiri CCM baadaye, aliahidi baada ya uchaguzi huo, ataandaa semina kwa ajili ya viongozi wa chama ili kuweka mambo sawa.

Alisema anamkakati wa kuwashawishi viongozi wakuu wa CCM kwenda kuvunja makundi hayo. "Mategemeo yangu baada ya uchaguzi ni kuwa wamoja na kuachana na makundi. Mimi naahidi kushirikiana na atakayeshinda kwenye nafasi ya Mwenyekiti wa Chama Wilaya, kwa sababu wote ni wangu na sina ninaye mpambania aweze kushinda," alisema Dk. Kiruswa.

Hivi karibuni, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdurahman Kinana, aliwaonya wagombea wanaochuana kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya CCM, kufanya kampeni za kistaarabu bila kuchafuana ili kuepuka chuki na mpasuko, baada ya uchaguzi kumalizika.

Alisema ndani ya uchaguzi lazima kutakuwa na makundi mbalimbali ya wagombea, hivyo wagombea wasitumie nafasi hiyo kufanya kampeni za chuki ambazo siyo za kistaarabu zinazoweza kuleta mgawanyiko mkubwa ndani ya chama.

Uchaguzi wa viongozi ndani ya CCM, Wilaya ya Longido, ulifanyika Oktoba mosi mwaka huu.




Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Proches Patrick, akiwaonyesha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii baadhi ya dawa zilizokamatwa zikiwa hazijasajiliwa na kutambuliwa ubora wake wakati walipofanya ziara ya kutembelea ofisi hizo, Arusha juzi, (kushoto kwake) ni Mkaguzi wa Dawa Kanda ya Kaskazini, Titus Malulu. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Uhaba madaktari bingwa mkojo, uzazi bado tatizo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa Maradhi ya Njia ya Mkojo na Uzazi (TAUS), Prof. Chalonde Yongolo, amesema Tanzania inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa wa upasuaji wa maradhi ya njia ya mkojo na uzazi.

Amesema kwa sasa idadi ya madaktari hao waliopo ni 100, kwamba hawakidhi mahitaji kulingana na idadi ya wagonjwa waliopo nchini.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kongamano la kisayansi na Mkutano Mkuu wa TAUS.

Prof. Yongolo alisema idadi ya madaktari bingwa katika sekta hiyo bado ni tatizo kwamba kwa idadi hiyo ni sawa na daktari mmoja kuhudumia wagonjwa 600,000.

"Tatizo la kutokuwapo kwa madaktari bingwa, liinachangiwa na kutokuwapo kwa mafunzo ya awali nchini juu ya masuala ya udaktari katika mfumo wa mkojo na uzazi.


"Hii ni kwa sababu mafunzo haya yalikuwa yanatolewa nje ya nchi, ila kwa sasa mafunzo hayo yameanza kutolewa rasmi nchini. Hivyo tunatarajia kupata idadi ya madaktari bingwa wa kutosha," alisema.

Alisema wanataka kuhakikisha wanakuwa na mikakati ya kuwa na madaktari bingwa katika kila wilaya ili kuziba pengo hilo.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema uwapo wa chama hicho, utasaidia kutoa elimu kwa jamii, juu ya matatizo hayo na kuona umuhimu wa kuwaona wataalamu mapema kwa ajili ya kupunguza ukubwa wa tatizo.

Katibu Mkuu wa TAUS, Dk. Degratius Mahenda, alisema watu wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea, ndiyo wanakabiliwa na tatizo la mfumo wa mkojo na uzazi na hiyo ni kutokana na wengi wao kutokuwa na elimu ya kutosha ya kuwahi kuona wataalamu, kabla ya tatizo hilo kuwa kubwa zaidi.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mfumo wa Mkojo, Uzazi kwa Wanaume na Upandikizaji wa Figo, Dk. Victor Sensa, alisema wamejipanga kuhakikisha wanahamasisha vijana wengi waliopo vyuoni, kujiunga na fani hiyo, huku wakiiomba serikali iwanunulie vifaa kwani viliyopo ni vichache havitoshi.





## Wanafunzi Korea wachangia mil. 100/- ujenzi wa madarasa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WANAFUNZI 27 raia wa Korea wamechangisha zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia kumaliza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Njoro iliyoko Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Shule ya Kikristo ya Saeronam ya Korea, Sung Hee, alisema wanafunzi wake wenye umri wa miaka 15 na 17, waliguswa na tatizo hilo baada ya kuwaona watoto wenye uhitaji, wakitafuta misaada ya kujengewa madarasa, hivyo kuamua kuwasaidia wenzao kuondokana na adha hiyo.

Upatikanaji wa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu ya Kituo cha Huduma ya Mtoto na Kijana ya Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Mailisita umeratibiwa na Shirika la Kimataifa la Compasion-Tanzania.

Mwezeshaji wa Ushirikiano kutoka TAG, Mercy Kimaro, alisema hali ilikuwa mbaya kabla ya kupatikana kwa msaada huo, kwa kuwa wanafunzi wa kituo hicho ambao wengi wao ni wale wasio na uwezo, hawana vyumba vya madarasa ya kusomea.

Mwakilishi wa Shirika la Compasion International Tanzania (CIT) katika shughuli hiyo, Mary Mwabukusi, alisema raia hao wa Korea, wamekuja nchini kushiriki shughuli za mikono, kwa ajili ya kuonyesha ufadhili wao wa majengo ili kanisa liweze kuwahudumia watoto wahitaji katika eneo hilo.

"Compassion ni shirika la kimataifa lililojikita katika maendeleo na utetezi wa mtoto. Dhamira yetu ni kuwakomboa watoto katika umasikini. Hadi kufikia sasa, CIT linafanya kazi na makanisa zaidi ya 520, huku watoto zaidi ya 112,000 wakifadhiliwa kwenye huduma za afya na elimu," alisema Mwabukusi.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mailisita, Elshadai, Semu Bukuku, alisema kituo hicho kina mkusanyiko mkubwa wa watoto wenye uhitaji na wasio na uwezo kutoka vijiji na mitaa mbalimbali, ambao wanahitaji misaada ya hali na mali ikiwamo kuwezeshwa kielimu.

# NEST 360 kupunguza vifo watoto wachanga

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WIZARA ya Afya imesema imeweka jicho la karibu katika mradi wa NEST 360, unaolenga kulisaidia taifa kufikia malengo ya kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 500 katika vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2025.

Mkuu wa Idara ya Mtoto wa Wizara ya Afya, Dk. Felix Bundala, aliyasema hayo juzi, wakati Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Seif Shekallaghe, alipotembelea na kukagua utekelezaji wa shughuli za Mradi wa NEST 360 katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Dk. Shekallaghe, aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Abbas Kayanda.

Alisema: "Sasa ili kufikia malengo hayo, zipo afua mbalimbali ambazo zinatakiwa kutekelezwa. Kwanza, lazima huduma muhimu kwa watoto wote wachanga wanaozaliwa waweze kuzipata.

Aliongeza: "Lakini, tunatakiwa hospitali zetu ziwe na wodi maalum kwa ajili ya kulaza watoto wachanga. Watoto wote wanaozaliwa, asilimia 20 watahitaji kulazwa na kwa Tanzania inakadiriwa kwamba watoto milioni mbili huzaliwa kila mwaka.

"Kwa asilimia hiyo 20, ni karibu watoto 450,000 wanahitaji kulazwa. Sasa kumekuwa na tatizo kwa hospitali zetu kutokuwa na maeneo maaalum kwa ajili ya kulaza watoto. Juhudi zaidi zinaendelea ili kufikia mwaka 2025 walao asilimia 80 ya hospitali zetu ziwe na vyumba hivyo."

Daktari Bingwa wa Watoto kutoka Chuo cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Nahya Salim, alisema malengo yao ni kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka ilivyo sasa mpaka kufikia chini ya asilimia 50.

Alisema: "NEST 360 tumejikita katika kuboresha huduma za watoto wachanga wodini ili kuboresha afya ya mtoto mchanga. Bado vifo vya watoto wachanga vinachangia zaidi ya asilimia 47 ya vifo vyote vya watoto wa chini ya miaka mitano.

"Kwa nini tumeanzisha mpango huu? ukiangalia sasa hivi takwimu zetu nyingi zinaonyesha kabisa na Tanzania ikiwamo, asilimia 80 ya wanawake wanakwenda kujifungulia hospitali. Kwa hiyo kuna uhitaji mkubwa wa kuboresha huduma za watoto wachanga katika hospitali zetu."

Mradi wa NEST 360, unatekelezwa katika nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania, Kenya, Malawi na Nigeria.

Baada ya kukagua uboreshaji wa huduma uliofanywa na NEST 360, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, alisema ombi la serikali wadau hao wa afya ni ni kupanua wigo wa huduma hizo katika mikoa mingine nchini kwa sababu tatizo hilo ni kubwa.



Wazee wa Mkoa wa Singida wakiwa katika maandamano ya kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Ikungi juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Agoma kuhama nyumba inayodaiwa kupigwa bomu

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKAZI wa Kijiji cha Naibili, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Silvia Lyimo, amegoma kuhama na familia yake kwenye pagala la iliyokuwa nyumba yake inayodaiwa kulipuliwa kwa bomu na polisi.

Inadaiwa kuwa polisi walilipua nyumba ya mama huyo wakitaka kumkamata mumewe, Pancras Shirima anayetuhumiwa kwa mauaji.

Akizungumza na Nipashe jana nyumbani kwake, mama huyo, alisema hataondoka katika pagala hilo hadi hapo atakapojua hatima yake na familia yake kwa kuwa polisi wameamua kumtia umaskini kwa makusudi.

Alisema: "Kutokana na manyanyaso niliyoyapata kutoka kwa polisi saba, waliokuja nyumbani kwangu na kulipua nyumba yangu kwa bomu, siwezi kuhama hapa mpaka nijue napataje haki yangu.

"Hali yangu ndiyo hii ya umaskini na ninavyoongea hadi sasa sijui mume wangu alipo. Kwa hiyo sioni haja ya kuondoka eneo hili, licha ya kuwa ni hatarishi kwa maisha yangu na mtoto wangu."

Polisi wa Kituo cha Sanya Juu, wilayani humo, wanadaiwa kuvamia makazi ya mwanamke huyo wiki iliyopita, wakimtafuta mume wake (Shirima) anayekabiliwa na tuhuma za mauaji, lakini hawakufanikiwa kumkamata na badala yake mmoja kati ya polisi hao alijeruhiwa kwa panga usoni.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Siha, Thomas Apson, askari aliyejeruhiwa wakati alipokwenda kumkamata mtuhumiwa huyo ni Wilfred Kavishe.

Kavishe ambaye yuko mahututi amelazwa katika hospitali ya wilaya hiyo.

Alisema tukio hilo lilitokea Septemba 27 mwaka huu, majira ya usiku katika Kijiji cha Naibili, baada ya polisi hao wakiambatana na Mwenyekiti wa Kijiji na Mtendaji wa Kijiji hicho, kufika nyumbani kwa mtuhumiwa wa mauaji yaliyotokea hivi karibuni kwenye kijiji hicho.

Akifafanua zaidi kuhusu tukio hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Naibili, Sabastian Shirima, ambaye ni ndugu wa Pancras Shima, anayedaiwa kumjeruhi askari huyo, alisema alipigiwa simu na saa 6:00 usiku na wananchi kwamba kuna askari polisi wakiongozana na Mtendaji Kijiji pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji cha Naibili, Benedict Mallya, wamefika nyumbani kwa mdogo wake kumkata kwa tuhuma za mauaji.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Melikiao Patrick, akisimulia mkasa huo alisema: "Nilipigiwa simu na polisi muda wa saa 2:00 usiku, kwamba wanakuja kijijini.

Aliongeza: "Walipofika walisema kuna watu kadhaa, wanawatafuta kwa tuhuma za mauaji na wakatutaka kwenda kwa Pancras Shirima. Tulipofika tuligonga mlango lakini mtuhumiwa aligoma kufungua mlango, ndipo askari huyo aliposukuma mlango na kujikuta akikatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na damu nyingi kuvuja.

Alisema: "Baada ya kuona damu, mimi nilikimbilia kwenye gari ya polisi na baada ya muda nikaona moshi ukifuka kwenye nyumba hiyo. Wakati wa purukushani hizo mtuhumiwa alifanikiwa kukimbia na kutokomea kusikojulikana."

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Yahaya Mdogo, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alikiri askari wake kujeruhiwa kwa panga kichwani nakusema amelazwa Hospitali ya Wilaya ya Siha.

NIPASHE JUMATATU OKTOBA 3, 2022

Nipashe

# Spotika



VIUNGO BORA WANAODHIBITI MTIRIRIKO WA MCHEZO DIMBANI UK.16



## ISIKUPITE

KEVIN De Bruyne kwa sasa ameifungia timu yake ya taifa mabao 25. Eden Hazard (33) na Romelu Lukaku (68), ni wachezaji pekee wenye mabao mengi zaidi yake katika timu yao ya Taifa ya Ubelgiji.

# KIHUNZI...

Mshambuliaji wa Arsenal, Mbrazili Gabriel Martinelli, akiruka kihunzi cha beki wa kati wa Tottenham, Muargentina Cristian Romero wakati wa mechi ya Ligi Kuu England, 'London 'Dabi'' iliyopigwa Uwanja wa Emirates jana na Arsenal kushinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**



# WACHEZAJI WA5 'VIRAKA' UWANJANI

**LONDON,** England

INGAWA makocha wanatafuta kila wakati kupata wachezaji waliobobea katika kila nafasi, umuhimu wa mchezaji mwenye uwezo mwingi hauwezi kupuuzwa. Wachezaji soka ambao wanaweza kucheza vizuri katika nafasi nyingi (viraka) ni mali ya thamani kwa timu zao.

**Wanasoka wengi huishia kucheza katika nafasi ambazo hazikutumika sana katika miaka yao ya ujana. Ujuzi walioupata, pamoja na uwezo wao wa asili, unawasaidia kukua na kuwa wanasoka wenye nyanja nyingi, uwezo wa kutoa majukumu mbalimbali kwa ajili ya pande zao.**

Ni vigumu kwa mchezaji yeyote katika ngazi ya juu kuzingatiwa kuwa wa kiwango cha kimataifa katika nafasi moja. Lakini kuna wachezaji ambao wamethibitisha kuwa wa ajabu katika nafasi nyingi. Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji watano wanaocheza nafasi tofauti uwanjani...

**#5. BERNARDO SILVA (URENO/ MANCHESTER CITY)**

Bernardo Silva alijiunga na Manchester City kutoka AS Monaco kama winga mzuri wa kulia. Lakini kutokana na ufinyu wake wa kasi, alihamishwa nafasi na kocha wa City, Pep Guardiola. Silva alibobea katika nafasi yake kama namba nane ambaye alikuwa na uhuru mwingi wa kuzurura mbele na kuvamia safu ya tatu ya mashambulizi.

Kwa miaka mingi, mchezaji huyu wa kimataifa wa Ureno, amekuwa na ufanisi katika majukumu mengi. Anafanya vema kama winga wa kulia kutokana na uwezo wake bora wa kuhifadhi na kuendeleza mpira. Uamuzi wa Silva, udhibiti wa karibu na kupiga pasi sahihi kunamfanya kuwa mmoja wa wachezaji hatari zaidi wa Man City katika nafasi ya tatu ya mwisho.

Anaweza kucheza kama kiungo wa kati, namba tisa na kama winga wa kulia kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England. Katika mechi 10 kwenye michuano yote aliyoichezea Manchester City hadi sasa msimu huu, Silva amefunga mabao mawili na kutoa asisti tatu.

**#4. IVAN PERISIC (CROATIA/TOTTENHAM HOTSPUR)**

Ivan Perisic alikuwa sehemu ya kikosi shujaa cha Croatia kilichotinga fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2018. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye alijiunga na Tottenham Hotspur msimu huu wa majira ya joto, ana uwezo wa kucheza katika nafasi nyingi na ni mmoja wa wachezaji mahiri katika mchezo hivi sasa.

Perisic anaweza kucheza kama mshambuliaji na kiungo mkabaji. Perisic pia anaweza kucheza upande wa winga zote mbili na hii inamfanya kuwa mchezaji bora zaidi.

**#3. FEDE VALVERDE (URUGUAY/ REAL MADRID)**

Fede Valverde ambaye ni mahiri, amejitambulisha haraka kama mmoja wa wachezaji wa kutegemewa wa Real Madrid.

Akili yake ya mchezo, pamoja na uwezo wake bora wa kiufundi, sasa umemfanya kuwa chaguo la kwanza kwenye kikosi cha kwanza cha Real Madrid.

Huku Real Madrid ikikabiliwa na uhaba wa viungo wa kiwango cha kimataifa, Valverde mara nyingi hutumika kama winga wa kulia. Anafanya vema katika nafasi hiyo na huwatisha mabeki kwa kasi yake na ujuzi wa ajabu.

Katika mechi tisa kwenye mashindano yote kwa 'Los Blancos' hao hadi sasa msimu huu, Valverde amefunga mabao manne na kutoa asisti mbili.

**#2. DAVID ALABA (AUSTRIA/ REAL MADRID)**

David Alaba alikuwa na msimu mzuri wa kwanza katika klabu ya Real Madrid baada ya kujiunga na klabu hiyo msimu wa majira ya joto wa 2021. Beki huyo mahiri alishinda mataji ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya katika msimu wake wa kwanza akiwa na 'Los Blancos' hao.

Alaba ni mchezaji mahiri kiufundi ambaye anaweza kucheza katika nafasi nyingi. Alitokea Bayern Munich kama beki wa kushoto. Wakati huo huo, alikuwa akitumika kama kiungo wa kati wa timu ya Taifa ya Austria. Akawa mzuri sana katika nafasi zote mbili.

Katika ngazi ya klabu, Alaba amebadilika taratibu na kuwa beki wa kati ambaye uwezo wake bora wa kucheza mpira unaisaidia timu yake kucheza kutoka nyuma kwa raha. Bila shaka ni mmoja wa wanasoka hodari zaidi kwenye sayari hii.

**#1. JOSHUA KIMMICH (UJERUMANI/BAYERN MUNICH)**

Joshua Kimmich amejidhihirisha kuwa mmoja wa viungo bora wa kizazi chake. Amekuwa katika kiwango kizuri kwa Bayern Munich katika hatua za mwanzo za msimu mpya. Kimmich ni kama gwiji wa Ujerumani, Philipp Lahm, anakumbukwa kwa kubadilika kutoka beki wa kulia hadi kiungo wa kati katika siku zake za mwisho za uchezaji kabla hajastaafu na sasa ni Kimmich.

Kimmich alikuwa akicheza kama kiungo wa kati wakati wa miaka yake ya mwanzo. Lakini aliwekwa kama beki wa kulia katika miaka yake ya awali akiwa na timu ya wakubwa ya Bayern chini ya uongozi wa Pep Guardiola. Uwezo wa hali ya juu wa kiufundi wa Kimmich umemwezesha kucheza nafasi zote mbili kwa ufasaha.

Kimmich amecheza kwa kiasi kikubwa kama kiungo wa kati siku za hivi karibuni na ni nadra sana kutumika kama beki wa pembeni. Anafanya vema katika uchezaji wake.




Twaha Kiduku akiwa ulingoni dhidi ya bondia kutoka Misri, Abdo Khaled.

# TWAHA KIDUKU NA SIRI NZITO ULINGONI

**Na Saada Akida**

“Sijawahi kuhofia bondia yeyote yule pamoja na kuchagua mtu wa kucheza naye kwa sababu nafanya maandalizi kulingana na mtu ambaye nitacheza naye kulingana na uzito,” ndivyo anavyoanza kueleza Bondia Twaha Kassim Rubaha maarufu Twaha Kiduku alipofanya mazungumzo maalum na Nipashe mkoani Mtwara hivi karibuni.

**Kiduku ambaye asili ya familia yake kwa upande wa baba ni mkoani Pwani katika Kijiji cha Kiparang’anda wilayani Mkuranga, anasema kutokana na ukweli kwamba ngumi ni kazi yake, yuko fiti na tayari kupanda ulingoni dhidi ya bondia yeyote ambaye atahitaji kucheza naye.**

Anasema alikuwa mwigizaji na mcheza ngoma za asili nyumbani za mikao mbalilmbali ikiwamo marimba na kabla hajajikita katika ngumi, bondia aliyekuwa akimvutia alikuwa Muhammad Ali ambapo kutokana na kufuatilia mapambano yake, yalimfanya kushawishika zaidi kujikita katika ngumi na kusahau masuala mengine yote maishani mwake.

**UFALME WAKE**

“Kila jambo ni Mungu sikujua kama nitafikia hivi, maana nilichukulia ngumi kama ubabe tu, lakini baada ya kujikita zaidi na kuwekeza nguvu na akili zangu katika mchezo huu sasa nimefikia hatua hii,” anasema bondia huyo ambaye makazi yake kwa sasa ni mkoani Morogoro.

Anasema pambano lake la kwanza kupigana alipewa Sh. 20,000 kipindi ambacho anaishi na baba yake mzazi (marehemu) na aliona pesa nyingi hasa kutokana na maisha ambayo alikuwa akiishi na mzee wake.

Kiduku mwenye rekodi ya kucheza mapambano 29 likiwamo la Septemba 24, mwaka huu ambalo alishinda kwa pointi dhidi ya Bondia kutoka Misri, Abdo Khaled, anasema kati ya hayo ameshinda jumla ya mapambano 20, nane akiibuka na ushindi kwa KO na amepoteza nane kati ya hayo moja ni kwa KO huku akitoka sare mara moja tu.

Katika pambano lake la mwisho dhidi ya Mmisri huyo, Kiduku alifanikiwa kutwaa ubingwa wa UBO, Uwanja wa Nagwanda Sijaona, Mtwara.

**MTAZAMO WAKE KATIKA NGUMI**

Kiduku anasema kwenye ngumi za kulipwa zimekuwa na umaarufu mkubwa na sehemu kubwa ya ajira kwa vijana wenye vipaji vya masumbwi.

“Ngumi kwa sasa ni mchezo wenye heshima kubwa na ni kazi kama zilivyo kazi zingine zinazowaingia watu vipato,” anasema.

**MALENGO**

Kiduku anasema malengo yake ni kufika mbali zaidi na ikiwamo kuiletea sifa nchini yake kupitia mchezo huo wa ngumi za kulipwa ambao kwa sasa unakua kwa kasi hapa nchini.

“Kila mmoja huwa na malengo yake, binafsi nahitaji kukua katika mchezo huu zaidi ya nilipo sasa, kuwa tishio katika mataifa mengine,” anasema bondia huyo ambaye mipango yake baada ya kuachana na ngumi ni kuonyesha nini alichokipata kupitia mchezo huo.

“Kikubwa namshukuru Mungu kwa nafasi hii aliyonipa, nitajitahidi kuitumia vizuri hata kama itakuja kuisha na kuja wengine, basi nijue ngumi imenipa nini na nini.

“Lakini pia nina malengo ya baadaye kuanzisha kituo cha vijana kujifunza ngumi. Nilikuwa nayo hata kabla sijajulikana maana nilianza kufundisha kabla ya kufundishwa ngumi wakati nikiwa sijui chochote katika mchezo huu.

“Namshukuru Mungu baadaye nilikutana na mwalimu Pawa Iranda Jeuri ya Tanzania akanipa ujuzi zaidi.”

**FAMILIA YAKE**

Kiduku anasema familia yake imekuwa na mchango mkubwa katika kumuunga mkono na wanamtia moyo kila anapokwenda kupambana, jambo ambalo limekuwa hamasa kubwa kwake ya kupata ushindi.

## Extra Time



KROOS

# VIUNGO BORA WANAODHIBITI MTIRIRIKO WA MCHEZO DIMBANI

**LONDON,** England

WANASEMA kuwa mechi nyingi za mpira wa miguu hushinda kwenye safu ya kiungo cha kati. Ni ngumu kubishana na hilo kwa sababu kinachotokea katikati ya uwanja na timu gani inatawala hakika ina mchango mkubwa kwenye matokeo ya mchezo.

**Safu ya kiungo ni uti wa mgongo wa timu yoyote. Ni juu ya viungo kuweka mambo sawa wakati timu yao inamiliki mpira. Pia ni wajibu wao kuhakikisha safu yao ya kiungo haivunjiki kirahisi sana wakati hawana mpira.**

Kwa vile safu ya kiungo inaelekea kuwa eneo lenye watu wengi zaidi uwanjani, timu zinahitaji wachezaji wenye akili ya mchezo na uwezo mkubwa wa kiufundi. Hawa ni wachezaji ambao hawawezi kutikiswa na mpira kwa urahisi na wanaweza kuamuru mchezo kutokana na pasi zao.

Makala haya inawaangalia viungo watano wanaodhibiti mtiririko wa mchezo, haya sasa...

### #5. RODRI (MANCHESTER CITY)

Rodri anakaa chini ya safu ya kiungo ya Manchester City na anaendesha mambo kutoka katikati mwa uwanja kwa urahisi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania ni mpiga pasi mzuri wa mpira. Hanyang'anyiwi kirahisi na anatumia uwezo wake wa hali ya juu kuweka mpira kwenye nafasi zinazofaa.

Rodri ni mchezaji hodari ambaye ni mtulivu kwenye mpira na mara chache hupoteza. Ikiwa Manchester City itapoteza mpira, atakuwa tayari ameshaingia kwenye safu ya ulinzi kusaidia kuimarisha ulinzi.

Anaweza pia kuchangia mabao muhimu na amekuwa baraka kabisa kwa kikosi cha Pep Guardiola baada ya kuondoka Fernandinho.

Rodri amedumisha usahihi wa kustaajabisha wa pasi za asilimia 92.16 katika michezo sita ya Ligi Kuu iliyochezwa hadi sasa.

### #4. THIAGO ALCANTARA (LIVERPOOL)

Katika kilele cha nguvu zake, ilikuwa ngumu kupata mchezaji ambaye angeweza kudhibiti kasi ya mchezo bora kuliko Thiago Alcantara. Mchezaji huyo wa Liverpool ni mmoja wa wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu kwenye sayari hii. Ubunifu wa Thiago, pamoja na upigaji pasi wake sahihi, unamfanya awe karibu sana katikati ya uwanja.

Thiago anaweza kucheza popote kwenye eneo la kiungo na ana uwezo mkubwa wa kuhifadhi mpira. Anaamuru uchezaji kutoka kwa kina na ni furaha kumwona akibadilisha uchezaji haraka na kusogeza mpira kwenye nafasi zisizo na watu wengi ili kusaidia upande wake kumiliki mpira.

Kama si majeraha ya mara kwa mara, angeendelea kuwa mmoja wa wababe wa muda wote wa mchezo huo.

### #3. MARCO VERRATTI (PARIS SAINT-GERMAIN)

Kiungo wa kati wa Paris Saint-Germain, Marco Verratti ni mmoja wa wachezaji bora ambao hawatacheza Kombe la Dunia mwaka huu baada ya Italia kushindwa kufuzu. Verratti ni mmoja wa viungo bora wa kati wa zama za kisasa na licha ya kimo chake, anasimamia mambo katikati ya uwanja.

Udhibiti wa karibu wa Verratti ni wa hali ya juu.

Verratti, ambaye kimsingi ni mchezaji anayetumia mguu wa kulia, anaweza pia kucheza vizuri na mguu wake wa kushoto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, kwa urahisi ni mmoja wa viungo kamili zaidi katika mchezo hivi sasa. Verratti bila kushangazwa ana usahihi wa kupiga pasi kwa asilimia 94.22.

### #2. JOSHUA KIMMICH (BAYERN MUNICH)

Joshua Kimmich amekuwa mchezaji bora wa Bayern Munich hadi sasa msimu huu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, bila shaka ndiye mchezaji bora zaidi duniani. Anazurura katika eneo la kiungo na ni mmoja wa wachezaji waliocheza vizuri kwenye mchezo.

Anafanya vema katika kushinda mpira nyuma na pia ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa. Yeye huwa anatafuta nafasi za wazi na akili nyingi.

Mojawapo ya sifa zinazohitajika kwa mchezaji ni ujuzi wa kujua wakati wa kusonga mbele na wakati wa kukaa nyuma. Kimmich anafanya hivyo.

Katika mechi nane kwenye Bundesliga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, Kimmich amefunga mabao mawili na kutoa asisti nne. Ametengeneza nafasi 20 katika mechi hizo alizocheza.

### #1. TONI KROOS (REAL MADRID)

Toni Kroos anachukuliwa kuwa mmoja wa viungo bora wa wakati wote. Amekuwa na maisha ya kifahari kule Real Madrid na amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu katika vipindi vyao vya mafanikio zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kroos ni mmoja wa wapiga pasi sahihi zaidi katika historia ya mchezo huo. Maono yake, ubunifu, uwezo wake ni bora zaidi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, pia ana uwezo mkubwa wa kumiliki mpira na ana nguvu ya kuwazuia wapinzani.

Kroos anacheza kana kwamba anaona kila kitu kinachotokea uwanjani. Anapunguza kasi na kuwaacha Real Madrid wajipange upya na kurejesha sura yao kila wakati. Kroos ataingia kwenye historia kama mmoja wa viungo bora zaidi wa wakati wote.

Kross amekamilisha pasi 278 kwenye LaLiga akiwa na pasi za uhakika za asilimia 94.56 ambazo ni pamoja na pasi ndefu 21 zenye mafanikio. Pia ametengeneza nafasi nane kwenye michezo hiyo.

## Nukuu

"Hii ni mara yangu ya pili kufunga bao kwenye mechi za 'dabi', mara ya kwanza ilikuwa dhidi ya Argentina [dhidi ya Brazil], bila shaka ni mwenye furaha, nataka kufunga katika kila mechi," **Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus baada ya kufunga bao dhidi ya Tottenham juzi wakishinda 3-1 kwenye Ligi Kuu England.**



"(Kevin) De Bruyne ndiye 'Shetani Mwekundu' (timu ya Taifa ya Ubelgiji), ninayempenda zaidi. Ninapenda mtindo wake. Sawa, yeye si mpiga chenga kama Eden Hazard, lakini ana mbinu nzuri," **Nguli wa zamani wa Brazil na Barcelona, Ronaldinho.**



"Ninakumbuka miaka 20 iliyopita wakati nikianza kucheza, lazima niseme kwamba nimeridhishwa sana na yote niliyoweza kuyafikia. Hii si kwa heri, ni mwanzo wa safari nyingine, sura nyingine ya maisha yangu. Natarajia siku zijazo na natumaini mtaendelea kuniunga mkono," **Nyota wa zamani wa Chelsea na aliyekuwa nahodha Nigeria, John Obi Mikel akitangaza kustaafu kucheza soka la ushindani akiwa na umri wa miaka 35 wiki iliyopita.**





Kikosi cha Al Hilal Omdurman kitakachopambana na Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi wiki hii kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: MTANDAO**

# UNDANI WAPINZANI SIMBA, YANGA CAF

**Na Adam Fungamwango**

WIKIENDI hii timu nne za Tanzania zitakuwa kwenye kibarua kizito cha kujaribu kusonga mbele hatua moja ya michuano ya kimataifa wakati zitakaposhuka dimbani kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

**Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga na Simba watakuwa dimbani mmoja akiwa ugenini na mwingine nyumbani kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Azam FC na Kipanga wao wakiwa wanaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.**

Hizo ni mechi za raundi ya kwanza ya michuano hiyo, na timu tatu kati ya hizo zimevuka vihunzi vya mechi zilizopita, huku Azam FC pekee ndiyo itakuwa inacheza kwa mara ya kwanza, msimu huu kwani iliingia moja kwa moja kwenye raundi hiyo.

Makala haya yanakuletea historia, rekodi na mambo usiyoyajua kuhusiana na wapinzani wote wanne watakaocheza na timu za Tanzania, twende sasa...

### AL HILAL OMDURMAN (SUDAN)

Mabingwa Yanga Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kunako majira ya saa 10:00 jioni, watakumbana na timu hii yenye maskani yake nchini Sudan, kabla ya kurudiana jijini Khatoum Oktoba 16, mwaka huu.

Al Hilal ni timu ambayo kwa misimu mitatu mfululizo imecheza hatu ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Ilifanya hivyo msimu wa 2019/20, 2020/21 na 2021/22, na iwapo itashinda basi itaweka rekodi ya kutinga hatua hiyo mara nne mfululizo.

Kama itatolewa na Yanga, basi itarudia kile kilichoitokea msimu wa 2017/18 na 2018/19 ilipotolewa kwenye raundi ya kwanza. Kwenye misimu yote matatu, timu hiyo iliyoanzishwa mwaka 1920, huwa inaishia kwenye makundi tu na haijawahi kupita na kwenda hatua ya robo fainali.

Inanolewa na Florent Ibenge, kocha Mkongomani ambaye msimu uliopita aliiwezesha timu ya RS Berkane ya Morocco kutwaa Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kwa bahati mbaya sana kwa timu hiyo, bado mpaka sasa nchini kwao ligi haijaanza, ingawa hivi karibuni ilianzisha mashindano ili kuwaweka wachezaji wake kwenye hali nzuri ya kimichezo na kuialika Simba na Asante Kotoko.

Mechi yake ya kirafiki dhidi ya TP Mazembe imeota mbawa baada ya baadhi ya wachezaji wa timu hiyo ya Congo kufungiwa, hivyo kuhofia waliopo kupata majeraha.

### PRIMEIRO DE AGOSTO (ANGOLA)

Wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, Simba watakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Estadio 11 de Novembro nchini Angola Jumapili wiki hii majira ya saa 12:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki na ya marudiano inatarajiwa kupigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Oktoba 16.

Timu hiyo ya Angola iliyoanzishwa mwaka 1977, ilishika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya nchi hiyo kama Simba msimu uliopita.

Iliitoa Red Arrows kwenye mechi raundi ya awali kwa kushinda ugenini nchini Zambia bao 1-0, kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani Luanda, Angola. Kwenye mechi yake ya ufunguzi wa Ligi Kuu msimu huu imetoka suluhu nyumbani dhidi ya Cuando Cubango mechi iliyochezwa Septemba 28, mwaka huu, huku jana Jumapili ilitarajiwa kucheza dhidi ya Bravos do Maquis.

Mafanikio yake makubwa kwenye Ligi ya Mabingwa ni kutinga hatua ya nusu fainali ilipofika nusu fainali mwaka 2018, na ilifika hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirishisho Afrika mwaka 2009.

### AL AKHDAR SC (LIBYA)

Timu hii kutoka nchini Libya, ndio wapinzani wa Azam FC kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Azam ambayo haikucheza mechi hatua ya awali, itaanzia ugenini kwenye Uwanja wa Martyrs Februari nchini humo majira ya saa 2:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki na mechi ya marudiano itapigwa nchini Oktoba 14, mwaka huu.

Ni timu ambayo haina historia yoyote nzuri kwenye michuano ya kimataifa, ingawa ilianzishwa tangu 1958. Mwaka 2006 ilitolewa kwenye hatua ya awali na 2008, itafanikiwa kuvuka hatua moja zaidi na kuondolewa kwenye raundi ya kwanza ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Mpaka sasa Ligi nchini Libya haijaanza.

### CLUB AFRICAIN (TUNISIA)

Klabu hii kubwa na maarufu kwenye soka la Afrika itacheza na wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Kipanga ya Zanzibar.

Ni klabu ya mataji kwani iliweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza nchini Tunisia kutwaa ubingwa wa Afrika mwaka 1991.

Klabu hiyo kongwe iliyoazishwa mwaka 1920 na kuwa na miaka 102 sasa, pia ilitwaa ubingwa wa Bara la Asia mwaka 1991/92, na Arab Cup mwaka 1995 na 1997. Timu hiyo itacheza mechi yake ya kwanza kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar Jumamosi wiki hii majira ya saa 10:15 jioni kwa saa za Afrika Mashariki kabla ya kurudiana nchini Tunisia Oktoba 14, mwaka huu.

Je, nani ataanza vizuri mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ili kurahisisha kazi katika mchezo wa marudiano? Wikiendi si mbali, tusubiri tuone.

NDANI YA 18



PENALTI aliyofunga Harry Kane wakati wakichezea kichapo cha mabao 3-1 dhidi ya Arsenal juzi, inamfanya kuipiku rekodi ya Thierry Henry ya kuwa mfungaji bora wa wakati wote kwenye mechi za Dabi ya London kwa Ligi Kuu England baada ya kufikisha mabao 44 aliyozifunga timu zote za London. Lakini akimpiku Henry kwa kufunga mabao 14 sasa dhidi ya timu hizo (Arsenal vs Spurs) zilipokutana.

# SOKA




**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Erling Braut Haaland
**KUZALIWA:** Julai 21, 2000 (Miaka 22)
**ALIPOZALIWA:** Leeds, England
**TIMU YA TAIFA:** Norway
**KIMO:** 1.95 m (6 ft 5 in)
**NAFASI:** Straika
**KLABU:** Manchester City
**JEZI NAMBA:** 9
**MABAO:** 12 (Ligi Kuu England) 2022/23 kabla ya jana dhidi ya United

Nipashe **Spotika**

WANASEMA kuwa mechi nyingi za mpira wa miguu hushinda kwenye safu ya kiungo cha kati. Ni ngumu kubishana na hilo kwa sababu kinachotokea kati-kati ya uwanja na timu gani inatawala hakika ina mchango mkubwa kwenye matokeo ya mchezo.

**Uk. 16-17**

# WACHEZAJI WA5 BORA WA LALIGA MSIMU HUU



LEWANDOWSKI

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, 2022-23 umekuwa wa kuvutia hadi sasa, kwa kuwa tumeshuhudia maonesho mengi bora ya timu mbalimbali na baadhi ya matokeo ya kushangaza pia.

**Mabingwa watetezi, Real Madrid ndio vinara wa ligi kwa sasa, huku Barcelona, Real Betis, na Athletic Bilbao wakimaliza nafasi nne za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.**

Hata hivyo, timu kama Real Sociedad na Atletico Madrid zimekuwa na matokeo tofauti kidogo, huku Sevilla wakipoteza mechi tatu kati ya sita za mwanzo za msimu huu.

Katika michezo sita ya ufunguzi wa msimu, kuna baadhi ya wachezaji ambao wamefanya mambo ya kipekee. Kwa hiyo, makala haya inaangalia wachezaji watano bora wa LaLiga hadi sasa...

**#5. MARC-ANDRE TER STEGEN**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ujerumani amekuwa bora katika goli la Barcelona kwenye msimu unaoendelea wa 2022-23.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ndiye kipa mwenye idadi kubwa ya mechi alizocheza bila kuruhusu bao, na ameruhusu idadi ndogo ya mabao kwenye LaLiga msimu huu.

Ter Stegen kwa sasa ndiye mlinda mlango mwenye uwiano wa juu zaidi wa kuokoa katika ligi tano bora za Ulaya akiwa na asilimia 92.9 ya kuokoa.

Ter Stegen anabakia kuwa mchezaji muhimu kwa kocha Xavi katika msimu unaoendelea wa 2022-23. Ikiwa anaweza kudumisha uthabiti wake, ana nafasi kubwa ya kushinda tuzo ya golikipa bora (Golden Glove).

**#4. ALEX BALDE**

Hisia za kijana huyu zimekuwa za kipekee, na ubunifu wake umekuwa muhimu kwa Barcelona.

Balde mwenye umri wa miaka 18, ametoa pasi tatu za mabao katika mechi tano alizoicheza Barcelona, na ni mmoja wa wachezaji walio na asisti nyingi zaidi katika msimu unaoendelea wa LaLiga.

Ikiwa anaweza kubaki sawa na kile anacholeta kwenye timu, kuna uwezekano mkubwa kwamba atapata muda mwingi wa kucheza.

Raia huyo wa Hispania anasalia kuwa mchezaji muhimu kwa Xavi katika msimu huu wa 2022-23.

**#3. BORJA IGLESIAS**

Raia huyu wa Hispania amekuwa katika nafasi ya tatu ya mwisho ya uwanja kwa Real Betis katika msimu huu na kiwango chake kimeboresha matokeo ya Real Betis.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, hadi sasa amefunga mabao sita katika michezo sita, akiwa pia mfungaji bora wa pili katika msimu huu wa LaLiga.

Miaka mitatu nyuma, mashabiki wa Real Betis walikuwa hawamwamini Borja na walichoshwa na kutoaminika kwake.

Msimu uliopita, alifunga mabao 10 kwenye ligi katika mechi 33. Kwa haraka sana msimu huu - mabao sita katika mechi sita tayari na tuzo ya mchezaji bora wa mwezi.

Uchezaji mzuri wa Iglesias ulimfanya apate nafasi ya kuitwa Timu ya Taifa ya Hispania. Iglesias alitawazwa kuwa Mchezaji Bora wa Mwezi wa LaLiga wa Agosti 2022 akiwashinda Robert Lewandowski na Vinicius Jr.

Iglesias anasalia kwenye kinyang'anyiro cha kushiriki michuano ya Kombe la Dunia ijayo, na ni mchezaji muhimu wa Real Betis katika msimu unaoendelea.

**#2. VINICIUS JUNIOR**

Mbrazil huyo amekuwa na kiwango bora tangu msimu wa 2021-22 na bila shaka ndiye mchezaji aliyefanya vema zaidi Real Madrid katika msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ana mchango wa mabao saba katika mechi zake sita zilizopita akiwa na Real Madrid kabla ya mchezo wa jana.

Kutokana na kukosekana kwa Karim Benzema, ambaye ndiye mchezaji tegemeo wa Real Madrid kwenye safu ya ushambuliaji, Vinicius amefanya vema. Vinicius anasalia kuwa mchezaji muhimu wa Real Madrid katika msimu unaoendelea, na litakuwa jambo la kuvutia kuona kama ataendelea kuwa thabiti kwa msimu wote.

**#1. ROBERT LEWANDOWSKI**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland bila shaka ni mmoja wa washambuliaji bora katika historia ya soka, na amekuwa na kiwango bora kwa miaka mingi kadhaa.

Lewandowski kwa sasa ndiye mfungaji bora katika msimu unaoendelea wa LaLiga akiwa amefunga mabao nane katika michezo sita. Aidha, huu ni msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu Hispania.

Hii ina maana kwamba amezoea kwa haraka mtindo wa uchezaji wa Barcelona na LaLiga kwa ujumla. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, hadi sasa ameboresha uwezekano wa kufunga wa Barcelona na matokeo ya timu kwa ujumla.

Lewandowski anasalia kuwa mchezaji muhimu kwa Barcelona katika kampeni inayoendelea ya 2022-23.

**USILOLIJUA**



KATIKA Ligi tano bora Ulaya, Klabu ya Barcelona imeonyesha kuwa na safu bora ya ulinzi ikiwa imeruhusu bao moja tu katika mechi saba za LaLiga ilizocheza hadi sasa, lakini safu ya ushambuliaji haijalala kwani imeshatupia mabao 19 msimu huu.



## HABARI MBEYA

# RC aita wakulima mbolea ya ruzuku

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya wametakiwa kuendelea kujiandikisha kwenye maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya kunufaika na mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi akikagua usajili wa wakulima kwa ajili ya kunufaika na ruzuku hiyo kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Mayeka alisema kuanzia msimu huu mbolea itakuwa inauzwa na mawakala maalumu ambao wamesajiliwa kwa ajili ya kuuza tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ilikuwa inauzwa bila utaratibu mzuri hali iliyosababisha hasara.

Alisema kwa sasa wakulima wote wanasajiliwa kwenye mfumo maalumu wa serikali ili kila mbolea inayouzwa ijulikane mkulima aliyeinunua na mahali alipo kwa ajili ya kuzuia upotevu wa raslimali za serikali.

Alisema amebaini kwamba kuna mwamko mzuri kwa wakulima kujiandikisha hasa maeneo ya vijijini ambako ndiko shughuli nyingi za kilimo zinafanyika.

Hata hivyo aliwataka wasambazaji wa mbolea hizo kuhakikisha zinawafikia wakulima kwa wakati ili waendane na msimu wa kilimo na kwamba kuna baadhi ya maeneo mvua ikianza kunyesha inakuwa vigumu kufikika.

Alisema maeneo hayo wakulima wanatakiwa kupelekewa mbolea mapema ili hata barabara zikiharibika kusiwe na tatizo la usafirishaji wa bidhaa hizo.

Alisema kutokana na serikali kuweka ruzuku bei zimeshuka na kuuzwa kwa chini ya nusu ya bei ya msimu uliopita kwa maelezo kuwa kwa mwaka huu hakuna mbolea itakayouzwa kwa zaidi ya Sh. 70,000 tofauti na msimu uliopita, kwamba baadhi ya mbolea ziliuzwa mpaka Sh. 140,000.

# Uchelewaji ujenzi skimu wawapa hofu wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga wilayani Mbarali mkoani Mbeya wameingiwa na hofu ya kutoanza kwa wakati msimu ujao wa kilimo kutokana na kuchelewa kwa ujenzi wa skimu za umwagiliaji ambazo wanazitegemea.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa makabidhiano ya mikataba ya ujenzi wa skimu nne za umwagiliaji kati ya serikali na makandarasi ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwezi huu.

Mmoja wa wakulima hao, Jafary Mwinjuma alisema wakati wa ujenzi wa miundombinu hiyo ni lazima ile ya zamani ambayo walikuwa wanaitumia itavunjwa na hivyo kusababisha maji kutofika mashambani.

Alisema kilimo cha mpunga katika maeneo mengi ya wilaya hiyo wanategemea umwagiliaji na kwamba endapo miundombinu hiyo itachelewa lazima madhara yatatokea.

"Sisi wakulima wa Skimu ya Uturo miundombinu yetu itafumuliwa umbali wa mita 60, sasa hatujui kama watakamilisha kujenga ndani ya mwezi mmoja maana mpaka sasa bado hawajaanza hali ambayo pia inatupa wasiwasi kama tutalima mwaka huu ama la," alisema Mwinjuma.

Naye Emmanuel Kidolelo aliwaomba makandarasi waliopata zabuni ya kujenga miundombinu hiyo kuwashirikisha wakulima ili kuikamilisha kwa wakati na kilimo kiendelee kama kawaida.

Alisema wakulima hawana utaalamu wa kujenga miundombinu hiyo lakini kwa kuwa wana uzoefu wa kulima wanayajua maeneo korofi na hivyo wakishirikishwa itakuwa rahisi kwa makandarasi hao kuijenga kwa wakati na kwa ubora.

Alisema endapo makandarasi hao watategemea utaalamu wao pekee kuna hatari wakakwama kukamilisha miundombinu hiyo na mwisho wakawachelewesha wakulima kuendelea na shughuli zao.

Mwakilishi wa Tume ya Umwagiliaji Mkoa wa Mbeya, John Chacha, alisema kazi ambazo makandarasi hao watafanya ni kujenga mabanio, mifereji ya kupeleka maji shambani na mifereji ya upili kwenye mashamba.

Alisema mikataba hiyo minne ina thamani ya Sh. milioni 52 na kwamba makandarasi wote waliopewa kazi hizo ni wazawa.

Alisema watahakikisha wanasimamia ujenzi wa miradi hiyo kwa ukaribu ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa, huku akiwataka makandarasi kuepuka kufanya uhuni wa aina yoyote.

Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Juma Maditto, alisema serikali haitawaongezea muda makandarasi hao endapo watashindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na hivyo akawataka kuanza kujihami mapema.

Hivyo, aliwataka kuanza kupeleka vifaa muhimu vya ujenzi kwenye maeneo ya kazi ili kuepuka kushindwa kufikisha vifaa hivyo mvua ikianza kunyesha na kuchelewesha kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema katika wilaya hiyo kuna skimu za umwagiliaji 85 ambazo wakulima wanazitumia lakini zenye miundombinu mizuri zipo 34 pekee na kwamba baadhi ya skimu wakulima wamekuwa wakitumia miundombinu ya kienyeji.

Alisema kwa sasa serikali imepanga kuboresha skimu zote lakini kwa kuzijenga kwa awamu tofauti na hivyo akawataka wakulima kuendelea kujiandaa kuongeza uzalishaji.




Mjasiriamali wa dawa za kienyeji akiuza dawa iliyotengenezwa na mti wa mlonge kwa wateja wake eneo la Sokoine jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 'Kuwapo kipimo kutawabaini madereva wanaovuta bangi'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, amependekeza kutafutwa kwa kipimo maalumu cha kuwabaini madereva wanaotumia dawa za kulevya aina ya bangi na mirungi.

Amesema endapo wakibainika, wazuiliwe kuendesha magari kwa lengo la kuepusha ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

Alitoa pendekezo hilo juzi jijini Mbeya wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Mabalozi wa Usalama barabarani ambalo lilifanyika kitaifa na kushirikisha wadau mbalimbali.

Sagini alisema baadhi ya ajali zimekuwa zikisababishwa na madereva hao ambao wanakuwa wametumia dawa hizo za kulevya na hivyo weledi wa kuendesha magari kuwa mdogo.

Alisema kwa sasa askari wa usalama barabarani wana vifaa vya kuwapima madereva wanaokuwa wametumia pombe, lakini wanaotumia dawa hizo za kulevya kipimo hicho hakuna.

Naibu Waziri Sagini aliliagiza Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuweka mikakati endelevu ya kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya kutoa msaada wa haraka kwa majeruhi inapotokea ajali.

Alisema kukiwa na ushirikiano mzuri baina ya majeshi hayo vifo vinavyotokana na ajali za barabarani vitapungua tofauti na ilivyo sasa hivi, akibainisha kuwa baadhi ya watu wanakufa kutokana na kuhudumiwa na watu wasiokuwa na weledi.

Hivyo, aliyataka majeshi hayo kwenda pamoja kwenye maeneo zinakokuwa zimetokea ajali ili kutoa msaada wa haraka kwa waathirika wa ajali hizo na kuokoa maisha yao.

Baadhi ya mabalozi wa usalama barabarani walisema wamekuwa wakipeana mafunzo ya mara kwa mara ili kuwa na weledi wa kutoa elimu kwa watumiaji wote wa barabara ili kupunguza ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea.

Mwenyekiti wa Baraza la Mabalozi hao Taifa, John Seka, alisema kwa sasa wanapeana mikakati ya namna ya kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kukabiliana na ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na taasisi zingine zinazohusika na masuala ya usalama barabarani kutoa elimu kwa wananchi na kwa madereva.

Mwenyekiti wa Baraza la Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Rajab Ghuliku aliiomba serikali kuharakisha ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Igawa wilayani Mbarali mpaka Tunduma mkoani Songwe ili kupunguza ajali kwenye baadhi ya maeneo.

Alisema kwenye baadhi ya maeneo yenye miinuko mikali ukiwamo wa Inyala, kwamba ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara, inatakiwa kuipunguza kwa kuweka kona.

Alisema wananchi wengi wamekuwa wakipoteza maisha kwenye maeneo hayo na wengine kubaki na ulemavu wa kudumu hali ambayo inapunguza nguvukazi ya taifa.

Mwakilishi wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Adam Maro, alisema kwa sasa hali ya usalama barabarani inaimarika kutokana na elimu kuendelea kutolewa, pia kuboresha miundombinu.





## NIC yapata faida bil. 72/- miaka 4

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC) limetengeneza faida ya Sh. bilioni 72 katika muda wa miaka minne kutokana na mapinduzi katika masuala mbalimbali ikiwamo kujiendesha kidigitali.

Vilevile, shirika hilo limewahamasisha Watanzania kujiunga na bima mbalimbali wanazozitoa za mali, ajali na maisha.

Akizungumza waandishi wa habari jijini hapo jana kwenye banda la maonyesho la NIC lililoko kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Shirika hilo, Karim Meshack alisema faida hiyo imetokana na kufanya mapinduzi kwenye maeneo matatu ambayo ni rasilimali watu, ubunifu na kujiendesha kidigitali.

"Tulianza na rasilimali watu kwa kutafuta wataalamu ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji ni kijana mwenye jicho la kibiashara, mwanzo shirika lilikuwa linafanya kazi kama mashirika mengine pamoja na kupata vijana wenye weledi wa kufanya biashara,"alisema.

Kiongozi huyo alisema shirika limeimarisha mifumo kwamba kwa sasa linajiendesha kidigitali.

"Hivi sasa hauwezi kukutana na karatasi, shughuli zote zinafanyika kwa mfumo wa digitali na tunafanya kazi kwa wateja kwa haraka, tuna mtandao mkubwa tupo katika kila eneo na unaweza kupata huduma ukiwa nyumbani umelala," alisema.

Aliongeza kuwa: "Eneo la tatu ni ubunifu mfano tuna mafao mengi ikiwa ni pamoja na kufiwa, haina maana utaenda kuchukua zile fedha na ukifika wakati wa kupata mafao unapata vilevile."

Meshack aliwahamasisha Watanzania kujiunga na shirika hilo kwa kuwa wanalipa kwa wakati, kwamba ndani ya siku saba mteja anapata stahiki zake.

"Tupo kwenye mkutano huu wa mawakili kwa sababu ni wateja wetu na siyo mawakili tu tunawashauri watu waje kwenye majanga hakuna mtu ambaye anayatabiri tunahitaji kuwasaidia Watanzania," alisema.

# Waziri ataka orodha taasisi vinara wa kusababisha kesi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amewatwisha mzigo mawakili wafawidhi wa serikali, akiwataka kuandaa orodha ya kesi za madai za taasisi zao zinazoitia hasara serikali na watu waliosababisha hali hiyo.

Ameagiza taarifa hiyo imfikie Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kupitia Wakili Mkuu wa Serikali ndani ya siku 14.

Akifunga Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali jijini hapo mwishoni mwa wiki, Dk. Ndumbaro alisema kuna baadhi ya taasisi zimekuwa kiwanda cha kuzalisha kesi ambazo zinaitia hasara serikali.

"Taasisi nyingine zimekuwa kiwanda cha kuzalisha kesi na ili kuepusha serikali kuingia kwenye migogoro ni vyema viongozi wa wizara na taasisi za umma kuzingatia ushauri wa wanasheria na mawakili wa serikali wakashirikisha katika kutoa uamuzi," aliagiza.

Alisema migogoro imesababisha serikali kuwa na kesi na mashauri mengi.

"Kesi ni nyingi mpaka Wakili Mkuu wa S erikali anazidiwa kwa sababu taasisi nyingine zimekuwa ni viwanda vya kuzalisha kesi.

"Kwenye hili ninaomba nitoe maelekezo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia kwa Wakili Mkuu wa Serikali kila wakili wa serikali mfawidhi aandae orodha ya kesi zote za madai zilizopo kwenye taasisi yake na kubainisha chanzo na sababu za kesi hizo," alisema.

Pia alitaka katika ripoti ya kesi hizo waeleza gharama au hasara ambayo serikali inaweza ikaingia kwenye kesi hizo, nani amesababisha kesi hiyo kwa jina na cheo chake.

"Kuna wengine ni mabingwa wa kusababisha kesi halafu wanawaachia mawakili wa serikali wapambane, kesi inakuwa ya ovyo na ikishindwa lawama zinaangukiwa kwa Wakili wa Serikali kuwa ameuza kesi, aliyesababisha kesi yuko ofisini," alisema.

Pia aliwasisitiza kutunza siri za serikali na kujikita kwenye matumizi ya TEHAMA yanayozingatia sheria, weledi na maadili.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Dk. Eliezer Feleshi, alisema chama hicho hakina chochote cha kuwagonganisha na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) huku akionya kutoingiza siasa.

Dk. Feleshi alisema anajua kuna wanachama wa chama hicho ni wajumbe kwenye TLS na wataendelea kuwa wanachama wa chama hicho.

Alisema chama hicho kitakuwa na programu mbalimbali na TLS kwa sababu vyote ni vyama vyao na kuwataka mawakili wa serikali kuipenda TLS.



Daktari wa Meno na Kinywa wa Hospitali ya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, Dk. Rutta Wilison, akimfanyia uchunguzi wa kinywa na meno Leila Daudi mwanafunzi wa shule maalumu ya Chinangali, huduma hiyo ilitolewa katika Shule ya Msingi Nkuhungu jijini Dodoma kwa kushirikiana na Taasisi ya Special Olympics Tanzania. Kulia ni mzazi wa mtoto huyo, Halima Iddi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Maofisa, viongozi wa dini wateta malezi ya watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAOFISA maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na viongozi wa dini wamekutana kwa ajili ya kuweka mpango kazi wa pamoja katika utekelezaji wa Programu ya Malezi na Makuzi ya Watoto (PJT-MMMAM).

Mkutano huo ulifanyika mwishoni mwa wiki jijini hapo ukiandaliwa na shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya malezi na makuzi ya watoto la Action for Community Care (ACC) umefanyika mwishoni mwa wiki jijini hapo.

Akizungumza katika mkutano huo, Ofisa Mradi wa Mradi wa Watoto Kwanza, Magreth Mukama, alisema lengo la kuweka mpango kazi wa pamoja katika utekelezaji wa PJT-MMMAM ni pamoja na kutaka jamii ijue umuhimu wa makuzi ya mtoto.

Mukama alisema kwa kuwakutanisha wadau hao, wanachochea utekelezaji wa programu hiyo na hatimaye kujenga watu ambao watakuwa na tija katika taifa.

"Serikali inatekeleza PJT-MMMAM kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kwa hiyo leo tumewakutanisha wadau hawa tuweze kuwapitisha katika mwongozo," alisema Mukama.

Wakizungumza katika kikao kazi hicho, viongozi wa dini walisema programu hiyo imekuja kwa wakati muafaka na wao watatumia nafasi zao kuhakikisha elimu inafika kwa jamii.

Kuhani Raha Halisi wa Kanisa Halisi la Mungu Baba la wilayani Kondoa alisema kwa kutumia nafasi zao watahakikisha ujumbe wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto unafika kwa waumini kupitia nyumba zao za ibada.

Alisema: "Sisi viongozi wa dini tuna watu wengi na tunaaminika, kwa hiyo hili jambo limekuja kwa wakati muafaka na sisi tutahakikisha tunashirikiana na Serikali katika utekelezaji wa suala hili ili watoto wapate malezi ambayo yatawafanya wakue vyema na baadaye kuleta tija katika Taifa".

Ofisa Ustawi wa Jamii, Elizabeth Shoo kutoka Wilaya ya Kondoa alisema wakati wa utekelezaji wa programu hiyo utakidhi haja na kurejesha msingi wa malezi na makuzi ya watoto.

Alisema: "Siku hizi na huu utandawazi uliopo kila mtu amekuwa 'busy' wazazi wamejisahau jukumu lao la malezi wameliacha kwa wasichana wa kazi, u-busy wa kutafuta pesa umefanya wazazi hawajui hata kuhusu ulinzi na usalama wa watoto wao, lakini kwa ujio wa programu hii sasa wazazi watakwenda kuamka na kulea watoto kwa kufuata misingi iliyowekwa na kuwawezesha kukua kwa utimilifu wao".



## 'Maofisa habari tambueni majukumu yenu kazini'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Habari Maelezo Zanzibar, Hassan Khatibu Hassan, amewataka viongozi wa serikali kutambua umuhimu na majukumu ya maofisa habari na mawasiliano katika sehemu zao za kazi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na maofisa habari na mawasiliano wa serikali kujadili hatua waliyofikia ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Maofisa Habari wa Serikali Zanzibar (ZICOO).

Alisema kukamilika kwa usajili wa jumuiya hiyo kutasaidia viongozi wa taasisi kufahamu majukumu ya maofisa hao pamoja na kuzitatua kero zinazowakabili.

"Kero ziko nyingi na tutajitahidi kukabiliana nazo ili kuhakikisha maofisa wa habari wanasimamia majukumu yao ya kuielezea jamii kuhusu utendaji kazi wa taasisi zao," alisema.

Katibu wa jumuiya hiyo, Makame Khamis Mohamed alisema kuanzishwa kwa jumuiya kutasaidia maofisa wa habari kupata sehemu ya kufikisha matatizo yao na kuchukuliwa hatua zinazostahiki.

Alisema jumuiya hiyo itatoa tuzo kwa maofisa habari wanaofanya vizuri pamoja na kutoa mafunzo kwa maofisa hao ili kuhamasisha utendaji kazi.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Raya Hamadi alishukuu Idara ya Habari Maelezo kwa kuwaweka pamoja maofisa habari na mawasiliano wa taasisi za serikali kwa kuanzisha jumuiya hiyo, hatua ambayo itasababisha kuimarika kwa sekta ya habari nchini.

Alisema hatua hiyo itasababisha maofisa hao kuzitangaza taasisi zao ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na Serikali ya Zanzibar.

# Wanaharakati walalamikia watuhumiwa 'kufoji' umri

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANAHARAKATI wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wamelalamikia kuwapo tabia ya kubadilisha umri watoto wanaotuhumiwa katika kesi za udhalilishaji, tabia ambayo inafanywa na baadhi ya wazazi na watendaji wasiokuwa waaminifu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki kisiwani hapo, wanaharakati kutoka mikoa mitatu ya Unguja, walisema vitendo hivyo vimekuwa vikirejesha nyuma juhudi zao za kupambana na vitendo hivyo.

Uchunguzi uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar umebaini kesi sita ziliripotiwa katika mikoa hiyo kwa vipindi tofauti huku watuhumiwa wa vitendo hivyo wakibainika kurejesha umri ili Sheria ya Mtoto isiwatie hatiani.

Mwanaharakati Asya Fadhil kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja alisema pamoja na kuundwa kwa mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji, matumaini yao yanaonekana kufifia kutokana na kuwapo kwa udanganyifu huo.

"Kuna kesi ambazo tunazifahamu na zingine hatuzifahamu, kwa mfano kesi inayomhusu mtuhumiwa... (jina tunalihifadhi kwa sababu za kisheria) jina lake katika jalada la mahakama anaitwa ... (jina moja limebadilishwa) ambalo hata Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ilithibitisha suala hilo na kesi hiyo kupandishwa katika Mahakama ya Watu Wazima lakini baadaye waliirejesha katika Mahakama ya Watoto," alisema.

Baba wa mtoto anayedaiwa kunajisiwa na mtuhumiwa huyo, alisema hatua iliyofanywa na mahakama ya kuupinga ushahidi uliotolewa na DPP, haikutoa haki kwa kesi ya mtoto wake.

"Nilihangaika sana kufuatilia ushahidi wa cheti hicho cha halali cha kuzaliwa lakini mwisho wa siku jitihada zangu ziligonga mwamba, ninamwomba Rais aliangalie kwa kina suala hili ili mtoto wangu apate haki kutokana na kitendo alichofanyiwa cha unyama," alisisitiza mzee huyo.

Mwanaharakati katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Fatma Khamis alisema kesi tatu zilipatikana ambazo zina matatizo ya watuhumiwa kubadilisha umri ili waonekana ni watoto.

Msaidizi wa Sheria katika Mkoa wa Kusini, Hija Ame, alisema waliwahi kukumbana na kesi za aina hiyo lakini haikufika mahakamani na kuishia katika kituo cha polisi.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Huda Othman, alikiri kupokea malalamiko kuhusu shida inayolalamikiwa ya kubadilishwa kwa umri wa watuhumiwa.

Alisema baada ya kuifikisha mahakamani kesi tajwa, walitakiwa kupelekea ushahidi wa cheti kipi halali na kipi siyo halali, jambo ambalo lilishindikana.

"Kesi kama hii niliwahi kukutana nayo na nilifanikiwa kwa sababu nilipata cheti halali cha mtuhumiwa lakini hii ya ... (inayolalamikiwa) ilishindikana kupatikana uhalali wa cheti halisi cha mtuhumiwa,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Mohammed Ame Makame alisema ofisi yao haijawahi kupokea malalamiko ya aina hiyo isipokuwa hutakiwa na mahakama kutoa ushahidi wa uhalali wa kesi zinazoendelea katika mahakama mbalimbali.

Alisema tatizo la vyeti feki lipo ambavyo vilitengenezwa miaka ya nyuma mitaani lakini kwa sasa kuna sehemu chache wanaendelea kutengeneza vyeti hivyo.

Kaimu Mrajisi wa Mahakama Kuu Zanzibar, Salum Hassan Bakar, alisema tatizo la umri huwa linajitokeza mahakamani na mara nyingi huwatumia wataalamu wa afya kwa kuwapima meno na baadaye kuwaletea ripoti kama umri wake ni sahihi au la.

Alisema endapo kuna mtu ambaye ana malalamiko hayo ni vyema akafuata taratibu za kisheria kwa kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Alisema kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu kesi za udhalilishaji 189 zilifunguliwa katika Mahakama za Unguja na Pemba. Kati yake, 33 zilitolewa hukumu na 156 zinaendelea.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema jambo hilo halikubaliki kisheria na yeyote ambaye anagundulikana anapaswa kuchukuliwa hatua.

Hivyo, aliiomba serikali kuchukua tahadhari juu ya masuala hayo ili yasiendelea kutokea.



Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, akimsikiliza Kaimu Mwenyekiti wa Kikosi Kazi kinachokusanya maoni ya wadau kuhusu ujenzi wa maridhiano ya amani Zanzibar. Kikosi hicho kilifika ofisini kuwasilisha ripoti ya maoni ya wadau. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais aona jambo kwa kikosi kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema mapendekezo na maoni yaliyokusanywa na Kikosi Kazi Maalum kuhusu amani na demokrasia ya Zanzibar, ni uwekezaji mkubwa utakaoisaidia Zanzibar katika kuendeleza amani ya kweli.

Aliyasema hayo juzi ofisini kwake Migombani mjini Zanzibar akipokea ripoti ya Kikosi Kazi Maalum kinachokusanya maoni ya wadau juu ya ujenzi wa maridhiano na amani Zanzibar kinachoundwa na kujumuisha wadau mbalimbali wa demokrasia, dini na asasi za kiraia.

Alisema Zanzibar kwa muda mrefu imeonekana kwamba maridhiano ni ya wanasiasa pekee na kwamba kuwapo kwa jitihada hizo ni jambo muhimu litakalosaidia kuweka mustakabali bora wa Zanzibar.

Othman alisema kwamba jambo hilo linatoa nafasi kwa wananchi na wadau kutoa maoni yao juu ya kile wanachokitaka katika nchi na ni busara kwa serikali ichukue na kutekeleza matakwa ya wananchi juu ya mtazamo sahihi unaohusu mustakabali wa nchi yao.

Alisema kuwapo maoni hayo ni fursa muhimu ya kuendeleza demokrasia na amani ya kweli katika kuendeleza maridhiano na Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchini kuwa endelevu.

Alisema kwamba utekelezaji wa maoni hayo unahitaji sana wanasiasa na viongozi kubadili fikra na mtazamo wao juu ya masuala mbalimbali yanayoihusu nchi katika kujenga mustakabali bora na kujenga Zanzibar yenye amani na maendeleo.


Hata hivyo, alisema ni vyema kwa wanasiasa kuondosha zana mbaya kwenye kuangalia mfumo wa masuala kwenye ujenzi wa demokrasia zikiwamo taratibu na sheria za uchaguzi katika mtazamo wa kimageuzi ya kidemokrasia.

Alisema viongozi na wanasiasa, wananchi na wadau wengine ndiyo msingi muhimu wa kusaidia kujenga hatima njema ya Zanzibar katika kuyaendea masuala mbali mbali yanayohusu nchi yao.

Katibu wa kikosi kazi hicho, Suleiman Bajuni, alisema kikosi hicho kimefanya kazi ya kukutana na wadau mbalimbali na kupata maoni na mapendekezo yao muhimu ya awali juu ya kuimarisha demokrasia, amani kabla, wakati na baada ya uchaguzi nchini.

Alisema juhudi hiyo inalenga pia katika kupatikana maridhiano endelevu yanayojumuisha matakwa ya wananchi na kukubalika na wadau na hivyo kuchangia ustawi bora wa maendeleo ya nchi kidemokrasia.

Alisema baada ya rasimu hiyo ya maoni imeonekana kwamba kuna haja kubwa ya kuwapo kwa mabadiliko katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu sheria na taratibu za uchaguzi katika kuchangia na kujenga uzalendo ndani ya Zanzibar.





## 'Waajiri pimeni afya wafanyakazi wenu'

**Na Elizabeth Faustin,** MWANZA

MKAGUZI wa Afya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) amewataka waajiri kuwafanyia uchunguzi wa afya wafanyakazi wanaowaajiri kwa mara ya kwanza na pale wanapomaliza mikataba yao ya kazi.

Edwin Sengue alitoa agizo hilo mwishoni mwaka wiki wakati wa semina iliyohusisha waajiri na wafanyakazi kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE).

Semina hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu la OSHA la kuongeza uelewa kwa Watanzania kuhusu masuala ya afya mahali pa kazi.

Katika semina hiyo OSHA iliwasilisha mada mbili, moja ikijikita kuelezea Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 pamoja na dhana nzima ya usalama na afya mahali pa kazi.

Akiwasilisha mada hizo, Senguo alisema majukumu mengine ya OSHA ambao wapo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

Pia kufanya utafiti mbalimbali kuhusiana na masuala ya usalama na afya, pamoja na kuishauri serikali kuhusiana na uundaji wa sera katika eneo husika.

Baada ya kupokea mafunzo hayo baadhi ya washiriki waliahidi kuyafanyia kazi ili kulinda afya na maslahi ya wafanyakazi wote katika maeneo yao ya kazi.

Ofisa Elimu wa TUGHE, Nsubisi Mwasandende, alisema: "Tunawaomba OSHA waongeze nguvu zaidi katika ukaguzi kwenye maeneo ya kazi pamoja na kutoa ushauri kwa waajiri."

Mtumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Morogoro, Jackline Ngowi alisema:

"Kwa kweli mafunzo haya ni mazuri, lakini kutokana na ufinyu wa muda ni vyema wakatutembelea mara kwa mara katika maeneo yetu ya kazi na kutupatia elimu hii,"

Meneja wa Afya OSHA, Dk. Jerome Materu, alitoa wito kwa waajiri wote nchini kutumia vyema fursa ya mafunzo na ushauri wa kitaalamu unaotolewa na OSHA ili kuboresha mifumo ya usalama na afya katika maeneo ya kazi.

Alisema: "Kimsingi OSHA tumeendelea kutoa elimu ya usalama na afya mahali pa kazi ili kuwawezesha wadau wetu kutekeleza ipasavyo sheria pamoja na miongozo mbalimbali inayotolewa kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na hivyo kuleta tija katika uzalishaji."

# Wanaohujumu miradi ya maji wasababisha hasara mil. 130/-

**Na Vitus Audax,** SENGEREMA

MAMLAKA ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira wilayani Sengerema mkoani Mwanza (SEUWASA) inapoteza zaidi ya Sh. milioni 130 za mapato yake kutokana na hujuma zinazofanywa na baadhi ya watumiaji wa maji.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na maofisa kutoka SEUWASA pamoja na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Meneja Rasilimali Watu na Utawala wa SEUWASA, Musa Zabron alisema mpaka Septemba mwaka huu, walikuwa wamepoteza asilimia 50 ya mapato sawa na zaidi ya Sh. milioni 130.

Zabron alisema hujuma zinazofanywa na wateja hao ni pamoja na kutoboa mabomba na kujipatia maji kinyume cha utaratibu.

"Baada ya kuona tatizo hilo kama mamlaka tumefuatilia na kugundua kuwapo mwananchi mmoja aliyechimba tangi kubwa na kutoboa bomba la maji ili kuingiza maji humo bila kuhesabu matumizi ya maji hayo," alisema.

Aliongeza kuwa mtu huyo tayari amechukuliwa hatua na taratibu za kisheria zinaendelea, huku akiwataka wananchi wilayani humo kuendelea kutoa ushirikiano kwa mamlaka hizo ili kubaini watu kama hao ili kuboresha huduma ya maji kwa wananchi.

Fundi Usanifu wa RUWASA, Agnetha Samsoni, alieleza kuwa tatizo hilo limekuwa likitokea mara kwa mara kutokana na baadhi ya wananchi kutokuwa na uelewa juu ya hasara zitokanazo na uharibifu huo.

"Wananchi wamekuwa wakihitaji kupata huduma hii bure kwa kuharibu miundombinu ya maji hatua inayoisababishia hasara kubwa mamlaka, kama mamlaka tunazidi kufanya uchunguzi kwa kuwashirikisha wananchi juu ya utekelezaji wa huduma zetu kupitia vikundi mbalimbali kwenye jamii," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akiendesha trekta alipofungua kongamano la uzinduzi wa msimu wa kilimo 2022/2023 lililofanyika Wilaya ya Iramba. Anayeshuhudia uzinduzi huo kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro na (wa pili kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri avunja mkataba wa ujenzi mnada Malampaka

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesitisha mkataba wa ujenzi wa mnada wa Malampaka ulioko Kijiji cha Gurumwashi wilayani Maswa mkoani Simiyu baada ya mkandarasi kushindwa kuukamilisha kwa wakati.

Mkandarasi aliyekuwa anajenga mnada huo ni Kampuni ya Rumuli Engineering, ambayo ilishinda zabuni Januari mwaka huu.

Mnada huo ulipaswa kujengwa kwa Sh. milioni 261 na mkataba huo ulitakiwa kukamilika kwa muda wa miezi mitano.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea mradi huo, Waziri Ndaki alimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuvunja mkataba huo huku akilitaka Jeshi la Polisi kumkamata mkandarasi huyo na kumfikisha katika vyombo vya sheria.

"Lakini aweze kurudisha fedha za serikali alizochukua kwa kuwa wakati wa mkataba, mkandarasi alipewa kianzio cha Sh. milioni 44, lakini ameshatekeleza mradi huo kwa asilimia 9.2 sawa na asilimia 17 ya fedha aliyokuwa amechukua," alisema Waziri Ndaki.

Alisema mbali na mkandarasi huyo kushindwa kutekeleza mradi huo kwa muda uliopangwa, pia anadaiwa Sh. 500,000 kutoka kwa wafanyabiashara, vibarua na mafundi aliokuwa anafanya nao kazi.

Waziri Ndaki aliwataka makandarasi wa ndani kuacha kujiharibia kazi wanapoaminiwa na serikali, badala yake wafanye kazi kwa uadilifu na kwa ubora unaotakiwa ili waendelee kuaminiwa na serikali.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Maendeleo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, alisema serikali ilimwongezea muda wa miezi mitatu mkandarasi huyo lakini bado hakufanikiwa kumaliza kazi hiyo kwa wakati.

Fundi mkuu anayetekeleza mradi huo, Wambura Wiraki alisema sababu kubwa iliyosababisha washindwe kumaliza kazi hiyo kwa wakati ni pamoja na pesa kuchelewa kutolewa kwa wakati.

HABARI KIMATAIFA

# AU yalaani mapinduzi Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

MWENYEKITI wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU), Moussa Mahamat, amelaani mabadiliko ya serikali yaliyo kinyume cha katiba nchini Burkina Faso baada ya jeshi kumpindua Luteni Kanali Paul-Henri.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa juzi na AU, Mahamat alisisitiza kurejeshwa kwa utaratibu wa kikatiba nchini humo kabla ya Julai mosi, 2024.

"Mwenyekiti anatoa wito kwa wanajeshi kujiepusha mara moja na kitendo chochote cha vurugu au vitisho kwa raia, uhuru wa umma na haki za binadamu," ilisema taarifa.

**Tunaona kuwa kwa mara ya pili katika muda wa miezi minane, maofisa wa jeshi wamesema kuwa wamevunja serikali na kulifuta bunge na katiba.**

**WAITUHUMU UFARANSA**

Wakati AU ikitoa wito wa amani, inaelezwa kuwa waandamanaji wenye hasira wameshambulia ubalozi wa Ufaransa katika mji mkuu wa Burkina Faso, baada wa wafuasi wa wanajeshi waliofanya mapinduzi mapya kuituhumu Ufaransa kumpa hifadhi rais wa mpito aliyepinduliwa.

Kwa mujibu wa DW, waandamanaji hao walishambulia ubalozi huo uliopo katika mji mkuu wa Burkina Faso, Ouagadougou jioni ya Jumamosi baada ya kumpa hifadhi rais wa mpito aliyeangushwa Ijumaa ya wiki iliyopita.

Pia taarifa ilielezwa kuwa Ufaransa imekanusha vikali madai kwamba inampa ulinzi Rais huyo katika ubalozi wake na hata katika kambi zake za kijeshi, huku picha za video zilizowekwa katika mitandao ya kijamii zikionyesha kundi la watu wenye mienge inayowaka moto wakiwa katika eneo linalouzunguka ubalozi wa Ufaransa mjini Ouagadougou.

Inatajwa kuwa hadi kufikia Jumamosi jioni ilikuwa bado haijajulikana mahali alipo kiongozi huyo mwanajeshi aliyepinduliwa, huku Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa ikiendelea kukanusha madai ya kumpa hifadhi Rais huyo wa mpito.

"Tunakanusha rasmi kuhusika kwa aina yoyote ya matukio nchini Burkina Faso, Paul Damiba kamwe hajapewa hifadhi katika kambi zilizo na wanajeshi wetu, wala ubalozi wetu," ilisema wizara.

Aidha, kupitia mtandao wa kijamii wa twitter, wa Paul Damiba aliwataka wanajeshi walionyakua madaraka kwa kumpindua kutumia fikra timamu.

Msemaji wa serikali ya Ufaransa Anne-Claire Legendre, alisema wanalaani kwa nguvu zote ghasia zinazoelekezwa kwenye ubalozi wao na kuongeza kuwa kitengo cha dharura kimeundwa mjini Ouagadougou na kwamba watu wao wako tayari kuhakikisha usalama wa raia wa Ufaransa.

Kapteni Ibrahim Traore, ambaye alitambulishwa kama kiongozi wa mapinduzi mapya alionekana katika televisheni ya taifa Ijumaa jioni, na katika mahojiano yake ya kwanza, akisema yeye na watu wake hawana mpango wa kumdhuru Damiba.

"Kama tungetaka tungemkamata katika muda wa chini ya dakika tano, na pengine angeuawa katika mapigano, lakini hatutaki janga hilo, hatutaki kumdhuru rais kwasababu hatuna matatizo na yeye binafsi ila tunapigana kwa ajili ya Burkina Faso," alisema Traore.

Ilielezwa kuwa barabara za mjini Ouagadougou zimeendelea kufungwa na helikopta ilikuwa ikizunguka angani, huku tathmini ya ndani ya Umoja wa Ulaya (EU) ikionekana na shirika la habari la AP, ikisema kulikuwapo na shughuli za kijeshi zisizo za kawaida katika mji mkuu.

Marekani imejiunga na nchi zilizopaza sauti kulaani mapinduzi hayo ya kijeshi nchini Burkina Faso, ikidai kwamba yanayojiri yanaleta wasiwasi mkubwa.

"Tunaona kuwa kwa mara ya pili katika muda wa miezi minane, maofisa wa jeshi wamesema kuwa wamevunja serikali na kulifuta bunge na katiba," ilisema Wizara ya Mambo ya Nje ya Washington.**DW**



Kapteni Ibrahim Traore, ambaye alitambulishwa kama kiongozi wa mapinduzi mapya, akihutubia wanajeshi baada ya kutekeleza mapinduzi nchini Burkina Faso juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Kimbunga chasababisha vifo 20

**FLORIDA,** Marekani

MAJIMBO ya Florida, Kaskazini na Kusini Carolina nchini Marekani yametajwa kukumbwa na dhoruba kali ya kimbunga Ian na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 20 na uharibifu wa mabilioni ya dola.

Picha zilizotolewa juzi na idara ya taifa inayohusika na masuala ya Bahari na Anga zilionyesha nyumba kadhaa za pwani na jengo la hoteli lililokuwa karibu na kisiwa cha Sanibel cha Florida zilichukuliwa na maji, na kwamba nyumba zingine zilionekana kusimama huku zikiwa zimeharibiwa kwenye paa.

Kituo cha kitaifa kinachofuatilia kimbunga hicho kilieleza kuwa kilikuwa kinadhoofika, huku kikitabiriwa kuleta hali mbaya katika sehemu za majimbo ya Kaskazini na Kusini Carolina, Virginia na Magharibi mwa Virginia. **VOA**

## Vifo vyaongezeka machafuko Iran

**ZAHEDAN,** Iran

WATU 20 wakiwamo askari wa vikosi vya usalama wameuawa katika makabiliano ya silaha yaliyofanyika Zahedan Septemba 30, mwaka huu, huku waumini wakiandamana baada ya uvumi wa kubakwa kwa msichana mdogo na ofisa wa vikosi vya usalama.

Kwa mujibu wa maofisa wa mkoa huo, watu wenye silaha walishambulia vituo vitatu vya polisi katika mji wa Zahedan, na kuua takriban watu 20 na kujeruhi 20.

Gavana wa jimbo hilo alisema benki na maduka makubwa yalishambuliwa na waandamanaji waliokuwa na hasira, akieleza kuwa mwanzoni waandamanaji hao walirushia mawe kituo cha polisi, na baadaye kujaribu kuvamia vituo hivyo vitatu vya vikosi vya usalama.

Pia inaelezwa kuwa katika machafuko hayo, maofisa kadhaa wa polisi waliuawa pamoja na naibu mkuu wa idara ya ujasusi ya kikosi cha walinzi wa mapinduzi.

Gavana wa jimbo hilo alisema mashambulizi hayo yalikuja wakati maandamano mapya yakifanyika dhidi ya serikali katika miji miwili ya majimbo.

Katika taarifa ya Wizara ya Ujasusi ilibainisha kuwa katika maandamano hayo walikamatwa raia tisa wa kigeni wakiwamo wa Ufaransa, Uswisi, Italia, Poland na Uholanzi, pamoja na watu 200 wanaohusishwa na makundi ya upinzani, ya Mujahidina wa Watu, wanamfalme na ya Wakurdi yenye silaha. **RFI**

## Russia yawaondoa wanajeshi wake Lyman Ukraine

**MOSCOW,** Russia

WIZARA ya Ulinzi ya Russia imesema imewaondoa wanajeshi wake katika mji wa kimkakati wa Lyman mashariki mwa Ukraine.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na wizara hiyo, kutokana na sababu ya tishio la kuzingirwa, askari washirika waliondolewa kutoka Krasnyi Lyman hadi kwenye sehemu salama.

Aidha, pamoja na hatua hiyo vikosi vya Ukraine vilibainisha kwamba tayari vilishaingia katika eneo hilo ambalo wanajeshi wa RUssia walikimbia.

Vile vile, licha ya Russia kudaiwa kushikilia mikoa mimne ya Ukraine, inaelezwa kuwa Russia iliwaita wanajeshi wake walioshirikiana na wapiganaji wa ndani wanaoungwa mkono na Moscow. **BBC**

# Serikali yapigia debe kilimo cha mkataba

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wadau mbalimbali kuiga kilimo cha mkataba kinachofanywa na Kampuni ya Bia ya (TBL) kwa kuwa kinawapa wakulima uhakika wa masoko na kuwaondoa kwenye umaskini.

Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alitoa raia hiyo wakati wa kupokea taarifa kuhusu kilimo cha mkataba na uwezeshaji wa wakulima.

Kampuni ya TBL ndiyo imekuwa na mfumo wa kilimo cha mkataba na wakulima wa shairi, mtama na zabibu kwenye mikoa mbalimbali na kisha kununua mazao hayo yenyewe.

"Tumeona namna TBL inavyowajenga uwezo wakulima na kubadilisha maisha yao na sisi wizara tunataka kuona wakulima wanapata masoko kwa hiyo mfumo wa mkataba sisi ndiyo tunaoutaka ili wakulima waweze kuwa na uhakika wa masoko.

"Huu mfumo tunauunga mkono na tunataka kampuni zingine zinazotaka malighafi ziige kwasababu mfumo unampa uhakika mkulima. Wamesaidiwa kupata ujuzi na kujengewa uwezo wa kufahamu aina za mbegu na mbolea na wamepata fursa ya kupata mikopo," alisema.

Naibu waziri alisema serikali ina mkakati kabambe wa kuujengea uwezo wakala wa uzalishaji wa mbegu Tanzania na kushirikisha sekta binafsi katika kuzalisha mbegu za aina mbalimbali.

Alisema serikali itaweka maeneo mengi ambayo yatatumika kwa kilimo cha umwagiliaji ili iwe rahisi kuzalisha mbegu na kutatua changamoto hiyo kwa kipindi chote cha mwaka bila kutegemea msimu wa mvua.

Mkurugenzi wa TBL, Jose Ramirez, alisema kupitia mradi wa kilimo bora, TBL ni mhamasishaji mkubwa wa mnyororo wa thamani kwenye kilimo na kuhakikisha kwamba unamfaidisha mkulima kwenye mazao yake makuu ya mtama, shayiri na zabibu.

"Mradi wa kilimo bora una lengo la kufikia asilimia 100 kwenye ujuzi, muunganiko na uwezeshaji wa kifedha miongoni mwa wazalishaji wa TBL kufikia mwaka 2025," alisema.

Alisema TBL ilianza kutoa zabuni kwa wakulima mwaka 2019 na imefanikiwa kuwashirikisha wakulima 4,524 kutoka Dodoma, Arusha na Manyara huku wakishirikiana na taasisi za utafiti, bima na fedha na asasi za kiserikali.

Alisema ushirikiano huo umesababisha uzalishaji wa tani 15,233 kutoka kwa wakulima na kwamba kilimo bora kinawasaidia wakulima, lakini kinasaidia kufikia malengo makubwa zaidi endelevu.

"Kwa mfano, kinasaidia katika kufanikisha malengo endelevu ya kimaendeleo katika Umoja wa Mataifa ya kutokomeza njaa, kuwezesha upatikanaji wa chakula na lishe bora na kuboresha kilimo na kuhakikisha matumizi endelevu na mifumo ya uzalishaji," alisema.

Aliongeza kuwa kilimo hicho kinasaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake na kuboresha ushirikiano ili kufikia malengo ya dunia na kwamba utafiti, ufahamu, teknolojia na ufadhili wa kifedha ndio funguo za kubadilisha kilimo kwa kiwango kikubwa.

Alisema TBL imezingatia hayo ili kuleta maendeleo endelevu ya kilimo na mchango wa wakulima wa Tanzania kupitia mavuno bora, ufanisi wa rasilimali, afya ya mchanga na mapato ya wakulima wadogo.

Alisema mradi wa uchambuzi wa mnyororo wa thamani kwenye kilimo bora unazingatia kuonyesha na kuwasilisha matokeo ya athari za kijamii na kiuchumi katika minyororo ya thamani ya kilimo.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kushoto), akimsikiliza ofisa mauzo wa Kampuni ya GF Trucks &Equipments Ltd, Poul Msuku, alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maonyesho ya madini yaliyofanyika mkoani Geita mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watanzania watakiwa kuwasomesha yatima

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKURUGENZI wa Shule ya Msingi Maasai iliyoko mjini Singida, amewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kusaidia watoto wa mitaani na wenye mahitaji maalumu ili kuondoa dhana kwamba kundi hilo ni wenye tabia mbaya, waliotengwa na jamii na hawastahili kusaidiwa.

Sophia Mungaya alitoa wito huo wakati wa mahafali ya wahitimu 35 wa darasa la saba wa shule hiyo yaliyofanyika wiki iliyopita.

"Usifikiri mtoto wa mtaani ni mtoto mbaya sana, aliyepoteza mwelekeo, mwizi na asiyejifahamu, hapana wengi wana akili sana lakini sema wamekosa mkono wa watu wa kuwasaidia ili wapate elimu itakayokuwa msaada maishani mwao," alisema.

Mungaya alisema shule hiyo ilishaanzisha utaratibu wa kuwasaidia watoto wa mitaani kwa kuwasomesha, na kwamba kila mwaka wanachukuliwa watoto 11 wanaosomeshwa kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

Alisema watoto hao wanawapa kituo cha Upendo, Amani na ofisi ya Ustawi wa Jamii, na kwamba tangu 2006 zaidi ya watoto 50 wamesomeshwa na shule hiyo ambao baadhi wamefikia hadi elimu ya chuo kikuu.

Alisema wakati umefika kwa jamii kuamka na kutengeneza urafiki na watoto wao, ili kujenga mahusiano bora yatakayotengeneza malezi mazuri ambayo yatafunga milango ya watoto hao kukimbilia mtaani.

Mungaya alisema kuwa tatizo lililopo jamii ya Watanzania imekuwa haina utaratibu wa kuwasaidia watoto wa mitaa na kuwaona kama wametengwa na sio sehemu ya jamii yetu kitu ambacho kinawafanya baadhi yao kukata tamaa ya maisha.

Mkurugenzi huyo aliwataja wanafunzi wa darasa la saba wasikate tamaa na wasiwe na hofu watakapoingia kwenye chumba cha mtihani.

Mwalimu Mkuu wa shule huyo, Benard Ochieng', alisema wanafunzi hao wanaohitimu darasa la saba waliwaandaa vizuri kwa ajili ya mtihani wa taifa unaotarajia kufanyika wiki ijayo.

# Stanbic yazindua huduma maalum kwa wajasiriamali

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Stanbic Tanzania imezindua huduma maalum kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na kati, iitwayo 'Mpambanaji'.

Kaulimbiu ya huduma hiyo ni 'Tunakuwezesha Kukuza Biashara Yako' inayolenga wajasiriamali kufikia huduma za benki kirahisi na kupata fursa za uwekezaji nchini, kikanda na kimataifa.

Katika taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari, ilieleza kuwa, uzinduzi huo ulifanyika mkoani Mwanza juzi.

Mpambanaji inajumuisha huduma mbalimbali ikiwamo Akaunti mahusus kwa wajasiriamali (akaunti ya Mpambanaji mmoja mmoja, vikundi, na Saccos), huduma ya kujenga uwezo/ kuelimisha, huduma za kibenki bila mipaka, mikopo ya vyombo vya usafiri, huduma za bima, huduma ya kufanya biashara kati ya Tanzania na China, pamoja na huduma mpya ya Wakala wa Benki yenye zaidi ya mawakala 500 wanaoongeza uwapo wa huduma za benki nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara, Fredrick Max alisema:

"Sekta ya biashara ndogo na kati ni zaidi ya asilimia 70 ya sekta binafsi na inatoa ajira kwa zaidi ya watu milioni nne, kwa hiyo ina mchango mkubwa katika kuchangia uchumi wa Tanzania ikiwa zitarasimishwa."

Alisema: "Ndiyo maana kama taasisi ya fedha tumetambua umuhimu wa kuleta suluhisho ambalo ni zaidi ya usaidizi wa kifedha, kwa kuja na suluhisho ambalo litahakikisha wafanyabiashara wana zana wanazohitaji ili kuanzisha biashara endelevu na zenye faida."

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Omari Mtiga, aliweka wazi kuwa benki itaendelea kutafuta ufumbuzi pamoja na kubuni huduma zitakazokidhi kiu ya wateja wao.

Aliongeza kuwa wajasiriamali wanaweza kufungua akaunti ya Mpambanaji kwa kutumia TIN namba pamoja na Kitambulisho cha Taifa (NIDA).

Vilevile, akaunti hii haitakuwa na ada ya mwezi na kupitia akaunti hiyo mteja ataweza kuweka fedha, kutoa fedha na kufanya malipo.

# Shakira kizimbani Hispania

**BARCELONA,** Hispania

MALKIA wa muziki wa Pop kutoka nchini Colombia anayefanya kazi zake Marekani, Shakira anatarajiwa kupandishwa kizimbani kwa madai ya ukwepaji kodi.

Mahakama moja katika mji wa Barcelona nchini Hispania imeamuru Shakira kupandishwa kizimbani kukabiliana na mashtaka ya udanganyifu wa kodi inayokisiwa kufikia zaidi ya Euro milioni 14.


Shakira ambaye jina lake halisi ni Shakira Isabel Mebarak Ripoll, anakabiliwa na kesi hiyo baada ya kukwepa kodi kipindi anaishi nchini humo na mumewe, Gerard Pique mchezaji wa timu ya Barcelona ambaye alifunga naye ndoa mwaka 2011 na kutalikiana mapema mwaka huu.

Mahakama hiyo imeamua kuwa kesi hiyo inapaswa kufanyika, hata baada ya mwanamuziki huyo kulipa kiwango kilichodaiwa na Mamlaka ya Kodi ya Hispania, pamoja na riba ya Euro milioni tatu.

Julai mwaka huu, waendesha mashtaka walisema wangeliomba mahakama imuhukumu mwanamuziki huyo mwenye umri wa miaka 45, kifungo cha miaka nane jela.

Shakira anatuhumiwa kudanganya kwamba haishi Hispania, wakati alikuwa akiishi nchini huko pamoja na Pique.

Wawili hao, ambao wamezaa watoto wawili, walitangaza kutengana Juni mwaka huu.





# AMBER LULU ANATAKA MWANAUME MWENYE FEDHA

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Amber Lulu amechafua hali ya hewa baada ya kusema la moyoni kuwa hawezi kudumu kwenye uhusiano wa kimapenzi na mwanaume asiyekuwa na fedha za kutosha.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Amber Lulu amesema; "Siwezi kuwa na mahusiano na mwanaume asiyekuwa na fedha.

"Mimi ninahitaji kutunzwa na pia matunzo yangu yanahitaji sana fedha, sasa nitawezaje kudumu na mwanaume asiyekuwa na fedha?"

Ishu hiyo imesababisha Amber Lulu kushambuliwa na baadhi ya wanawake wenzake wakimtaka kutafuta fedha zake na kamwe asitegemee za mwanaume.

Taarifa za ndani zinadai kwamba, Amber Lulu na baba wa mtoto wake aitwaye, Emba Botion ambaye amejaliwa mtoto mmoja wa kike aitwaye Ariana, wameshaachana na chanzo kikidaiwa ni mambo hayohayo ya jamaa kutokuwa na 'mpunga' mrefu.

# *Queen Darleen afurahia kuacha ndoa*

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva kutoka familia ya WCB, Queen Darleen ameibuka na kusema kwamba acha watu wamwone mjinga baada ya kuachana na ndoa yake.

Darleen ambaye alifunga ndoa na mfanyabiashara Isihaka Mtoro kabla ya mambo kwenda mrama, anasema baada ya kuchukua hamsini zake, kwa sasa anaishi maisha yenye furaha kuliko wakati alipokuwa ameolewa.

Darleen amesema hayo wakati akitoa maoni yake kuhusu habari ya kusikitisha ya mwanamke wa Nigeria aliyefariki dunia wakati akikimbizana kwa gari na mume wake aliyekuwa na mchepuko ndani ya gari lingine

Mwanamke aliyefariki alikuwa mwanasheria ambaye imeelezwa kuwa alikuwa anapitia manyanyaso ndani ya ndoa na pia mumewe husika alikuwa hajatulia.

Inadaiwa pia kwa sasa aliyekuwa mume wa Darleen yupo na mwanamke mwingine ukiacha yule mke mkubwa, Sabra ambaye ilisemekana walimaliza tofauti zao za awali.



## HABARI MICHEZO

# AZAM YAWATAMANI WABRAZIL IKIIKARIBISHA SINGIDA BIG STARS

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Azam FC inatarajiwa kuikaribisha Singida Big Stars leo kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', ameeleza kuvutiwa na wachezaji wa Kibrazil akidai wana sifa zote za kuichezea timu yao kwenye michuano ya kimataifa.

**Akizungumza kuelekea kwenye mechi hiyo ya raundi ya sita ya Ligi Kuu, Zaka amewasifu Singida Big Stars kwa usajili mzuri wa wachezaji hao, lakini akasema wana kila sifa ya kuichezea Azam FC ili wacheze mechi za kimataifa.**

"Wamesajili vizuri, nitoe pongezi kwao na ni wachezaji hao ambao wanajivunia sana msimu huu, ila niwaambie viongozi wao kina Dismas Ten, Muhibu Kanu na wengine kuwa wale wachezaji wao wakae vizuri, tunaweza kuwapiga pigo takatifu, dirisha dogo linakuja, na siyo kama tunawatamani, naona kama wanastahili kuwa kwetu. Tutawaambia waje huku mpande basi la Iriza, huko mliko hamuwezi kucheza mechi za kimataifa," alisema Zakazi.

Aliongeza kuwa hayo yanaweza kufanyika pale Azam itakapoingia kwenye hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, alisema kama wakiwachukua watafuata taratibu zote na siyo kuwachukua hilolela.

Inawezekana Azam ikawa tayari imeshawamezea mate wachezaji hao, au ni kuwatoa mchezoni kwani leo zitakuwa Chamazi kucheza mechi za Ligi Kuu.

Zaka alisema ukiondoa hilo la Wabrazil wa Singida United, ndani ya uwanja timu hiyo pamoja na Azam FC zote zina wachezaji wazuri, hivyo kuifanya mechi hiyo kuwa kali na ya kusisimua, hasa baada ya wao kupoteza mechi kwa bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Ijumaa iliyopita.

Singida Big Stars ambayo imepanda daraja msimu huu, imekuja kivingine baada ya kuwashusha wachezaji kutoka Brazil na mmoja Argentina ambao uwezo na viwango pamoja na vipaji walivyonavyo vimeonekana kuvutia wengi kwa muda mfupi tu.

Baadhi ya wachezaji hao ni Peterson da Cruz, Rodrigo de Calvalho, Dario da Silva na Bruno Gomes.




Meneja wa Benki ya Azania Tawi la Tanga, Hajira Mmambe (wa tatu kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Tanga, Sebastian Masanja (wa pili kulia), baada ya kukabidhi vifaa vya michezo kwa timu ya mkoa huo inayoshiriki mashindano ya SHIMIWI Taifa yaliyoanza jana mkoani humo. Makabidhiano hayo yalifanyika katika Ofisi za Mkoa wa Tanga jana. **MPIGAPICHA WETU**

# *Black Sailor yataja inapojikwaa Ligi Kuu Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Black Sailor imesema wakati mgumu wanaopitia kwa sasa wa kutopata matokeo mazuri katika michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar ni kawaida hasa katika soka lenye ushindani, lakini tayari wamegundua ni wapi wanapojikwaa.

Black Sailor inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama moja katika michezo mitano waliyocheza wakifungwa minne na kutoka sare mechi moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Salehe Machupa, alisema kufanya vibaya katika mchezo wowote wenye ushindani ni kawaida hasa katika soka, hivyo kipindi hiki kigumu ambacho wanapitia wanaamini kitapita na timu hiyo itaweza kurudi katika kasi yake.

Alisema tatizo kubwa lililopo katika timu hiyo ni washambuliaji kushindwa kuzitumia nafasi wanazotengeneza na kupoteza umakini wakati wanapokuwa eneo zuri la kufunga.

Alisema timu hiyo inacheza vizuri katika dakika zote za mchezo, lakini changamoto ya umaliziaji ndio inasababisha kushindwa kupachika mabao licha ya kutengeneza nafasi nyingi za wazi.

"Tunatengeneza nafasi nyingi sana, lakini zote tunashindwa kuzitumia vizuri, hili ndilo tatizo kubwa tumeliona mpaka sasa, maana hata magoli tunayofungwa si mengi, mechi zote tumefungwa goli moja moja tu," alisema.

Aidha, alisema tayari wameanza kulifanyia kazi tatizo hilo kwa washambuliaji wake ikiwamo kuzidisha umakini pindi wanapopata nafasi ili waweze kuzitumia vizuri nafasi zote wanazopata.

Hata hivyo, amewataka mashabiki wa timu hiyo kutovunjika moyo na timu yao kutoka na mlolongo wa matokeo mabaya waliyoyapata tangu kuanza Ligi Kuu badala yake waendelee kuwapa hamasa wachezaji ili wafanye vizuri

Black Sailor inatarajia kushuka dimbani Ijumaa wiki hii kupepetana na Maafande wa KVZ katika mzunguko wa sita wa Ligi Kuu Zanzibar mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 11 jioni.

## Mtanzania ashinda tuzo ya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTANZANIA Samwel Malugu, amekuwa mtu mwingine aliyefanikiwa kuitangaza nchi hii katika tasnia ya urembo baada ya kushinda Tuzo ya Mbunifu Bora wa Mashindano ya Urembo ya Kimataifa kutokana na wazo lake la shindano la Miss Jungle International kukubalika na magwiji wa tasnia hiyo.

Tuzo hiyo iliyotolewa na Taasisi ya Kimataifa ya Tuzo za Ikoniki (IIA) yenye makazi yake nchini India, ilikuwa mahususi kwa ajili ya kuhamasisha vijana kuja na mchakato wenye tija kwa ajili ya kuendeleza sanaa ya urembo yenye kuzingatia heshima na maadili kwa jamii.

Malugu alishinda baada ya kuonyesha ubunifu wake bora wa shindano la kimataifa la Miss Jungle ambalo linatarajiwa kufanyika hapa nchini kuanzia mwishoni mwa mwaka huu kwa kuwahusisha warembo kutoka mataifa zaidi ya 30.

"Hii tuzo ni heshima, ila shindano la Miss Jungle International limeanzishwa likiwa na lengo la kuhamasisha utunzaji na uhifadhi wa mazingira pamoja na kutangaza utalii wa kimataifa," alisema Malugu.

Aidha, alisema tuzo aliyotunukiwa imempa hamasa na kupata chachu ya kufanya vizuri zaidi katika tasnia ya sanaa ya maonesho na utalii ulimwenguni kwa lengo la kuitangaza Tanzania kimataifa.

Shindano la Miss Jungle International litafanyika kwa mara ya kwanza Tanzania na kushirikisha warembo wa kimataifa kutoka zaidi ya nchi 30.

## Ruvu Shooting yanogewa Uhuru

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ruvu Shooting imeonekana kunogewa na Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam inaoutumia kama wake wa nyumbani, ikisema imekuwa ikifanya vema zaidi ikicheza hapo kuliko hata Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Charles Boniface Mkwasa, alisema ingawa uwanja wao ni Mabatini Mlandizi, lakini kisaikolojia tayari Uwanja wa Uhuru umekuwa kama wao wa nyumbani kwa sababu ya kuutumia mara kwa mara, na wachezaji wake hucheza vizuri sana na kupata matokeo mazuri.

Alhamisi iliyopita, Ruvu Shooting ikiwa kwenye uwanja huo inaoutumia baada ya ule wa Mabatini kufungiwa, iliichapa Coastal Union mabao 2-1.

"Sisi uwanja huu kisaikolojia ni kama wa nyumbani, na huwa tunautumia vizuri sana, tukicheza hapa, tunacheza vizuri kuliko hata tukiwa Mlandizi na hata kushinda," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### NEVEZ ANUKIA ARSENAL

ARSENAL wanatumaini kuipiku Liverpool na Manchester United kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo wa Wolves, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25. ***(Express)***

#### LANG AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya West Ham inapambana na AC Milan kuwania kumsajili winga wa Klabu ya Bruges, mwenye umri wa miaka 23, Noa Lang. ***(Calciomercato)***

#### HAALAND KUJAZWA NOTI

KLABU ya Manchester City itamwongezea mshahara Erling Haaland baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, kuanza vizuri msimu huu. ***(Star)***

#### MUDRYK KWA NICE

NICE inaongoza katika mbio za kumwania winga wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 22 licha ya kuwa pia anawaniwa na Brentford, Everton na Newcastle. ***(Sun)***

#### LAGE SHAKANI WOLVES

KOCHA wa Wolves, Bruno Lage majaliwa yake yapo shakani baada ya mwanzo mbaya kwenye Ligi Kuu England. ***(Telegraph)***

#### UNITED WAKOMAA NA JONG

KIUNGO wa Barcelona, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, bado anawaniwa na Manchester United. ***(ESPN)***

#### PEP HAFIKIRII MKATABA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema hafikiri kuhusu majaliwa yake kwenye klabu hiyo, licha ya mkataba wake kufikia tamati mwishoni mwa msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

#### DURAN ANYATIWA LIVER

KLABU ya Liverpool inamwania fowadi wa Colombia na Chicago Fire, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 18, lakini Chelsea inamtaka. ***(Sun)***

#### SCHJELDERUP AGOMBEWA

LIVERPOOL na Arsenal zinamwania straika mwenye umri wa miaka 18 raia wa Norway, Andreas Schjelderup, ambaye anaichezea klabu ya Nordsjaelland ya nchini Denmark. ***(Mail)***


#### HINCAPIE ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kumsajili mlinzi wa kati wa Bayer Leverkusen na Ecuador, Piero Hincapie, 20. ***(Teamtalk)***

#### BELLINGHAM ASHAURIWA

JORDAN Henderson na Trent Alexander-Arnold wamemshauri kiungo wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham kujiunga Liverpool. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI ANAWEZA KUTWAA TENA BALLON D'OR-KOCHA

**PARIS,** Ufaransa

KIWANGO cha Lionel Messi alichoonyesha dhidi ya Nice kinaweza kumfanya kuwa tena mchezaji bora wa dunia, kwa mujibu wa Kocha wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alianza kufunga katika ushindi wa mabao 2-1 wa PSG kwenye Ligue 1 Jumamosi kwa mkwaju wa faulo kutoka umbali wa yadi 22.**

Hilo lilikuwa goli la kwanza la mpira wa adhabu la moja kwa moja la Messi kwa PSG tangu ajiunge nayo kutoka Barcelona Agosti 2021 na la 60 katika maisha yake ya soka kwa jumla katika klabu na nchi.

> Anacheza vizuri na ana furaha kila siku anapofanya mazoezi, amekuwa na tabia ya kufunga...

Baada ya kuwa na msimu mbaya wa kwanza katika mji mkuu wa Ufaransa, Messi sasa ana mabao matano na asisti saba katika mechi zake tisa za kwanza za Ligue 1 msimu huu.

Na baada ya kusajili bao katika mechi mfululizo za ligi kwa mara ya kwanza akiwa mchezaji wa PSG, Galtier amemsifia mchezaji huyo ambaye ni mshindi mara saba wa Ballon d'Or.

"Nina furaha ya ajabu kumuona kila asubuhi mazoezini," alisema Galtier katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Anacheza vizuri na ana furaha kila siku anapofanya mazoezi.


"Ni mchezaji ambaye amekuwa na tabia ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja. Mwaka huu amerejesha ladha ya kufunga.

"Iwapo anaweza kuwa mchezaji bora zaidi duniani tena, ningesema ndiyo kwa sababu yuko katika umbo la ajabu na amejiandaa vya kutosha.

"Ana uhusiano na wachezaji wenzake ambao humfurahisha. Anapokuwa na furaha, anacheza; anapocheza, anaweza kufikia viwango vinavyoonekana katika maisha yake yote."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 360,
MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 5.51
X | 3.44
2 | 1.59
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP AKIRI BRIGHTON KUWABANA MBAVU




**LIVERPOOL,** Egland

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amekiri kwamba ilikuwa ngumu kwa timu yake kujiandaa kwa mechi ya Jumamosi dhidi ya Brighton kwa kuwa huu ulikuwa mchezo wao wa kwanza chini ya kocha Roberto De Zerbi.

Brighton walipata pointi iliyostahili baada ya kutoka sare ya mabao 3-3 kwenye Uwanja wa Anfield katika mechi ya kwanza ya kocha huyo wa Italia kwenye Ligi Kuu England.

Leandro Trossard alifunga mabao mawili kipindi cha kwanza kabla ya mawili kutoka kwa Roberto Firmino kusawazishia 'Wekundu' hao.

Akizungumza baada ya mechi, Klopp alifichua kwamba walitatizika kujiandaa na mchezo huo kwani hawakujua ni mbinu gani zitakazotumiwa na De Zerbi.

"Brighton ilijipanga kwa ujasiri sana," alisema Klopp.

"3-4-3, viungo wanne kwenye boksi, hatukuweza kujiandaa kwa hilo kwa sababu hatukujua wangefanya nini.

"Lakini hiyo ni mara nyingi sana katika soka. Una suluhu kwa hali fulani, lakini kabla hatujapata suluhu tayari tulikuwa tumefungwa bao 1-0, na hilo lilibadilisha kasi sana."

Liverpool sasa wamevuna pointi kumi pekee kutoka mechi saba za mwanzo.

"Tulihisi kama tumeshindwa, najua hatukupoteza, lakini ndivyo hivyo," aliongeza.

## Watu 174 wafariki vurugu za soka

**MALANG,** Indonesia

TAKRIBANI watu 174 wamefariki dunia katika mkanyagano kwenye mechi ya soka ya nchini Indonesia ambayo imekuwa mojawapo ya majanga mabaya zaidi kuwahi kutokea uwanjani duniani.

Watu wengine 180 waliumia vibaya baada ya timu ya nyumbani Arema FC kufungwa na wapinzani wao Persebaya Surabaya kwenye uwanja uliojaa watu Jumamosi nchini humo.

Mkanyagano huo ulitokea baada ya polisi kuwafyatulia mabomu ya machozi mashabiki waliovamia uwanjani.

Hofu ilipozidi kuenea, maelfu walisonga mbele kuelekea njia za kutokea za uwanja wa Kanjuruhan, ambapo wengi walikosa hewa.

Shahidi mmoja aliyetajwa kwa jina la Dwi, aliiambia tovuti ya Taifa ya Indonesia kwamba "niliona watu wengi wakikanyagwa" katika harakati za kutoka nje.

Ripoti za awali ziliweka idadi ya waliofariki kuwa takriban 130, lakini maofisa wa polisi baadaye walitangaza ongezeko kubwa ambalo liliweka idadi hiyo kuwa 174, huku watu 11 zaidi wakijeruhiwa vibaya.

Rais Joko Widodo ameamuru mechi zote za Ligi Kuu Indonesia zisitishwe hadi uchunguzi ufanyike.

Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), katika taarifa yake limesema kuwa polisi hawakupaswa kutumia mabomu ya machozi na imelaani tukio hilo.

Video kutoka uwanjani zinaonyesha mashabiki wakikimbia uwanjani baada ya filimbi ya mwisho kuashiria kufungwa kwa timu ya nyumbani 3-2, na polisi wakifyatua mabomu ya machozi kuwadhibiti mashabiki.

,499,520

# GWAMBINA MAMBO BADO MAGUMU CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Gwambina FC ambayo misimu miwili iliyopita ilikuwa Ligi Kuu, imeendelea kufanya vibaya kwenye Ligi ya Championship baada ya kuchapwa bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara dhidi ya Biashara United.

Gwambina haijashinda mechi yoyote mpaka kufikia raundi ya tatu ya ligi hiyo, ikiwa imefungwa mechi mbili na kutoka sare moja.

Ilichapwa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya Kwanza, na mechi iliyofuata ilikwenda sare ya bao 1-1 dhidi ya KenGold, kabla ya juzi kupokea kipigo hicho cha mabao 2-1.

**Unakuwa ni ushindi wa kwanza kwa Biashara United ambayo mechi zote mbili zilizopita ilipoteza. Ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Fountain Gate kwenye mechi ya kwanza na kupoteza kwa idadi kama hiyo dhidi ya JKT Tanzania.**

Kwenye mechi zingine za ligi hiyo zilizochezwa juzi, maafande wa Transit Camp nao walipata ushindi wao wa kwanza ilipoifunga African Sports mabao 3-1, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, na katika Dimba la Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam, Green Warriors ilidunguliwa bao 1-0 dhidi ya Mashujaa, Copco ikifungwa mabao 2-1 na ndugu zao wa mji mmoja Mwanza, Pamba, kwenye Uwanja wa Nyamagana, huku KenGold ikipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania, mechi ikipigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

**NGUMI...**



Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya KCB Tanzania, Christine Manyenye, akifuatilia mashindano ya ngumi ya Mo Boxing yaliyofanyika usiku wa Septemba 30, mwaka huu katika Ukumbi wa Mlimani City. Kwenye mashindano hayo, Ibrahim Class kutoka Tanzania alifanikiwa kuibuka na ushindi kwa kumchapa Alan Pina kutoka Mexico. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu (HR), Fauqiya Shareef. **MPIGAPICHA WETU**



# *Yanga yaonywa mechi Al Hilal*

INATOKA UKURASA 32

nyumbani na wanahitaji kupata matokeo lazima kuwaheshimu wapinzani," alisema Pluijm.

Kipa Metacha Mnata (pichani) alisema wao kama wachezaji wako tayari kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi muhimu licha ya ukweli kwamba Azam FC watakuwa nyumbani.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu tunahitaji kutafuta pointi kufikia malengo yetu, tunaenda kupambana kupata matokeo chanya dhidi ya wenyeji wetu Azam FC," alisema Metacha.

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/10/22 | 19:45 | Marseille vs Sporting Lisbon | 2.23 | 3.40 | 3.15 |
| 02. 04/10/22 | 21:45 | Plymouth vs Sheffield Wed | 2.56 | 3.26 | 2.61 |
| 03. 04/10/22 | 21:45 | Hartlepool vs Doncaster | 2.65 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 04/10/22 | 21:45 | Walsall vs Northampton | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 05. 04/10/22 | 22:00 | Porto vs Bayer Leverkusen | 2.20 | 3.49 | 3.14 |
| 06. 04/10/22 | 22:00 | Ajax vs Napoli | 2.20 | 3.69 | 2.99 |
| 07. 04/10/22 | 22:00 | Cardiff vs Blackburn | 2.48 | 3.19 | 2.74 |
| 08. 05/10/22 | 21:45 | Hull City vs Wigan | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 09. 05/10/22 | 21:45 | Rotherham vs Millwall | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 10. 05/10/22 | 22:00 | Sevilla FC vs Borussia Dortmund | 2.80 | 3.40 | 2.34 |
| 11. 05/10/22 | 22:00 | Preston vs West Bromwich | 2.86 | 3.21 | 2.39 |
| 12. 06/10/22 | 19:45 | Pyunik Yerevan vs Zalgiris | 2.40 | 3.22 | 2.92 |
| 13. 06/10/22 | 22:00 | Midtjylland vs Feyenoord | 2.89 | 3.64 | 2.23 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 03/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2031 | Fasil Kenema vs Adama City FC | 1.62 | 3.49 | 5.11 |
| 15:00 | 1517 | FK Radnicki Beograd vs FK Graficar Beograd | 4.70 | 3.38 | 1.69 |
| 16:00 | 1914 | AL Tora vs AL Karmel | 2.43 | 3.03 | 2.79 |
| 16:00 | 2347 | Coastal Union vs Kagera Sugar | 2.18 | 2.66 | 3.79 |
| 16:00 | 2471 | Mekelakeya vs Hadiya Hosahina FC | 2.60 | 2.80 | 2.80 |
| 16:00 | 2725 | FK Radnicki Sremska Mitrovica vs FK Novi Sad | 1.79 | 3.23 | 4.31 |
| 16:00 | 3894 | Al Ahli Amman vs Ittihad AL Ramtha | 2.27 | 3.05 | 3.00 |
| 16:00 | 4434 | Ittihad Shojaeyya vs Khadamat AL Nosirat | 1.36 | 4.32 | 7.66 |
| 16:00 | 4610 | OFK Vrsac vs Sloboda | 1.96 | 3.15 | 3.95 |
| 16:10 | 2417 | AL Musanaa vs Dhofar Salalah | 5.20 | 3.25 | 1.72 |
| 16:30 | 3374 | Kokand 1912 vs Surkhon Termez | 2.06 | 2.94 | 3.63 |
| 16:30 | 4536 | Lokomotiv Tashkent vs Neftchi Fargona | 1.69 | 3.34 | 4.81 |
| 17:00 | 1240 | Cukaricki St vs Radnicki Nis | 1.47 | 4.13 | 5.70 |
| 17:00 | 4685 | Baalama vs Kfarsoum | 2.24 | 3.19 | 2.94 |
| 17:30 | 2166 | MC Alger vs ASO Chlef | 1.66 | 3.30 | 5.12 |
| 17:45 | 4344 | AL Etihad vs Al Nasr Salalah | 4.61 | 2.99 | 1.82 |
| 18:00 | 3484 | PAS Giannina vs Panetolikos | 2.24 | 3.06 | 3.31 |
| 18:00 | 5605 | Botosani vs Universitatea Cluj | 2.71 | 3.06 | 2.61 |
| 18:15 | 2765 | Ruvu Shooting vs Young Africans | 5.51 | 3.44 | 1.59 |
| 18:30 | 5255 | Bouake FC vs Sporting Gagnoa | 6.87 | 3.63 | 1.47 |
| 19:00 | 1739 | Viimsi JK vs FC Nomme United | 2.09 | 4.34 | 2.77 |
| 19:00 | 2237 | IK Start vs Kfum Oslo | 1.86 | 3.59 | 3.54 |
| 19:00 | 2465 | Kryliya Sovetov vs FC Krasnodar | 2.11 | 3.51 | 3.11 |
| 19:00 | 2793 | Karmiotissa vs Olympiakos Nicosia | 2.32 | 3.28 | 2.98 |
| 19:00 | 2826 | Hapoel Petah Tikva vs Ironi Tiberias | 2.23 | 2.88 | 3.64 |
| 19:00 | 2899 | Chrobry Glogow vs OKS Odra Opole | 2.02 | 3.48 | 3.14 |
| 19:00 | 2937 | EN Paralimni vs Nea Salamis | 2.74 | 3.20 | 2.54 |
| 19:00 | 2961 | Grorud IL vs Raufoss | 3.54 | 3.59 | 1.86 |
| 19:00 | 4200 | Parnu Jalgpalliklubi vs FCI Levadia Tallinn U21 | 8.47 | 5.85 | 1.28 |
| 19:00 | 5006 | Macva Sabac vs FK Zlatibor | 2.07 | 3.10 | 3.60 |
| 19:00 | 5396 | Kongsvinger IL vs Sogndal | 2.09 | 3.54 | 2.95 |
| 19:00 | 5529 | Ranheim vs Sandnes Ulf | 2.07 | 3.60 | 2.96 |
| 19:00 | 5608 | Maccabi Jaffa vs Hapoel Kfar Saba | 3.67 | 3.02 | 2.14 |
| 19:00 | 5663 | Stabaek vs Aasane Fotball | 1.19 | 6.30 | 9.84 |
| 19:20 | 4772 | Al Salmiyah vs Kazma SC | 2.65 | 3.24 | 2.42 |
| 20:00 | 2168 | AEK Athens vs Ionikos Nikea FC | 1.21 | 5.84 | 13.09 |
| 20:00 | 2669 | Trelleborgs FF vs Jonkopings Sodra | 1.78 | 3.84 | 4.20 |
| 20:00 | 3970 | Fatih Karagumruk vs Istanbulspor | 1.69 | 3.82 | 4.52 |
| 20:00 | 4713 | Erzurum BB vs Denizlispor | 1.86 | 3.43 | 3.68 |
| 20:00 | 5173 | Nordsjalland vs Randers | 2.06 | 3.47 | 3.32 |
| 20:00 | 5253 | Slask Wroclaw vs Warta Poznan | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 20:00 | 5999 | IFK Varnamo vs Mjallby | 2.65 | 3.09 | 2.50 |
| 20:10 | 4747 | IFK Goteborg vs Elfsborg | 2.59 | 3.33 | 2.42 |
| 21:00 | 4483 | Chindia Targoviste vs Rapid Bucuresti | 3.35 | 3.05 | 2.20 |
| 21:45 | 1083 | Shelbourne vs St Patricks | 3.29 | 3.04 | 2.14 |
| 21:45 | 1695 | Verona vs Udinese | 3.05 | 3.40 | 2.19 |
| 22:00 | 2328 | Leicester vs Nottingham | 1.71 | 3.89 | 4.18 |
| 22:00 | 2691 | Rayo Vallecano vs Elche | 1.70 | 3.59 | 4.95 |
| 22:00 | 4497 | Zaragoza vs Eibar | 2.56 | 3.01 | 2.81 |
| 22:15 | 1469 | Maritimo vs Casa Pia Atletico | 2.81 | 3.11 | 2.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 3, 2022

Nipashe




## Messi anaweza kutwaa Ballon d'Or - Kocha

UKURASA 29

HAT-TRICK...



Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, akiifungia timu yake moja kati ya mabao matatu (hat-trick), aliyofunga wakati wakishinda 6-3 dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad jana. Mabao mengine matatu ya City yalifungwa na Phil Foden. **PICHA: MTANDAO**

## Twaha Kiduku na siri nzito ulingoni

**Na Saada Akida**

BONDI Twaha Kassim Rubaha maarufu Twaha Kiduku amesema hajawahi kumhofia bondia...



HABARI UK. 15

## Azam yawatamani Wabrazil wa Singida

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Azam FC inatarajiwa kuikaribisha Singida Big Stars leo kwenye Uwanja wa Azam...

HABARI UK. 28

# Yanga yaonywa mechi Al Hilal

## ● ● ● Ni wakati wakiivaa Ruvu Shooting leo, Morrison nje huku Mayele akiwa hatihati...

**Na Saada Akida**

WAKATI leo wakishuka dimbani kuivaa Ruvu Shooting kwenye Ligi Kuu Bara huku joto la homa ya mchezo wa kwanza wa hatua ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan likizidi kupanda, wachezaji wa Yanga wameonywa kuhusu mechi hizo mbili, imeelezwa.

**Leo usiku majira ya saa 1:00, Yanga itakuwa ugenini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwavaa wenyeji wa mchezo huo, Ruvu Shooting na baada ya hapo itashuka tena uwanjani hapo Jumamosi wiki hii kuikaribisha Al Hilal kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Katika mchezo wa leo, Yanga itawakosa wachezaji wao nyota watano kwa matatizo mbalimbali ambao ni Jesus Moloko aliyeumia katika mchezo wa Zalan FC, Khalid Aucho na Fiston Mayele wako katika uangalizi wa daktari wakiangaliwa kwanza hali zao katika mazoezi ya mwisho jana jioni, Bernard Morrison akitumikia adhabu huku Aziz Ki akizuiliwa nchini kwao kutokana na kuelezwa kupata maambukizi ya virusi vya corona.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema maandalizi yao yako vizuri na wanatia nguvu kwa wachezaji kuona umuhimu wa mchezo huu kwanza ili kupata pointi tatu.

Alisema mbali na ufundi lakini wamejiandaa kiakili kwa kuwataka wachezaji kuwaza mechi dhidi ya Ruvu Shooting ili kupata matokeo ya ushindi huku wakiwaonya kuacha kuwawazia Al Hilal kabla ya kumaliza mchezo huo wa leo.

"Ni mechi ngumu tumeongea na wachezaji kwanza kutafuta pointi tatu dhidi ya Ruvu Shooting, kabla ya mchezo wetu wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal.

"Tunawasisitizia wachezaji wasifikirie mechi ya Jumamosi dhidi ya Al Hilal, kwa sababu mechi ya kesho (leo) ni muhimu kupata ushindi katika mchezo wetu dhidi ya Ruvu Shooting," alisema Kaze.

Kuhusu Tuisila Kisinda, alisema atakuwa sehemu ya mchezo na kuwasaidia katika mechi hiyo ya kutafuta pointi tatu ili kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa.

Kwa upande wa beki wa Yanga, Dickson Job, alisema wamefanya maandalizi mazuri na wako tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu dhidi ya Ruvu Shooting.

"Wachezaji tunahitaji kujitoa kupata matokeo chanya na mechi yetu ya Ruvu Shooting ni maandalizi mazuri kuelekea mchezo wetu wa Jumamosi, muhimu ni kupata pointi tatu dhidi ya Ruvu Shooting kwanza," Dickson Job.

Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Frank Msese, akizungumzia mchezo huo, alisema kwa ujumla wako tayari kwa mchezo na anaimani zitakuwa ni dakika 90 ngumu.

Alisema wanawaheshimu Yanga kwa sababu ni mabingwa watetezi na hawajapoteza katika michezo 41 tangu msimu uliopita, lakini wamejipanga kupambana kwa hali yoyote kutafuta matokeo chanya.

"Mechi haitakuwa nyepesi kwetu na wala si rahisi kwa Yanga kwa sababu tumeona madhaifu yao na tutayatumia kutafuta pointi muhimu nyumbani," alisema Msese.

Mbali na mchezo huo mechi nyingine itapigwa katika Uwanja wa Azam Complex kati ya wenyeji, Azam FC na Singida Big Stars.

Katika mechi hiyo Azam FC itawakosa wachezaji wawili Bryson Raphael aliyepata majeraha katika majukumu ya timu ya Taifa na Issa Ndala.

Kocha Msaidizi wa Makipa wa Azam FC, Mwalo Hashim, alisema wamejiandaa vizuri dhidi ya Singida Big Stars kupambana kwa ajili ya kusaka pointi muhimu.

Alisema wanawaheshimu wapinzani wao na wataingia kwa tahadhari kubwa na kushuka na mipango na mbinu zao kwa ajili ya kupata ushindi.

"Tumepoteza mechi dhidi ya Tanzania Prisons, tumerejea uwanjani na kufanyia kazi makosa yetu, tupo tayari kwa ajili ya kupata matokeo mazuri nyumbani," alisema Mwalo.

Nahodha Msaidizi wa Azam FC, Cleophace Mkandala, alisema wamejiandaa vizuri na wamefanyia kazi madhaifu yao ya mechi iliyopita ili kutorudia dhidi ya Singida Big Stars.

"Tumejiandaa vizuri, hatutaki kurudia makosa yaliyopita katika mchezo dhidi ya Tanzania Prisons, makosa ya mechi hii hayatarudia katika mchezo dhidi ya Singida Big Stars na tunatumai kupata matokeo chanya," alisema Mkandala.

Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, alisema anajivunia kufanya maandalizi mazuri ya kiufundi dhidi ya Azam FC na anaimani utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu tumefanya maandalizi mazuri na tunahitaji matokeo mazuri, Azam FC wako

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >